# Utangulizi wa Elimu Mjumuisho kwa Jumuiya za Watu Wenye Ulemavu

Moduli ya

1



## Muongozo wa mwezeshaji


Umetayarishwa kwa ajili ya:

Jumuiya ya MECP-Z na Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

The Norwegian Association of Disabled

Umetayarishwa na:

Enabling Education Network, Agosti 2020


NAD - The Norwegian Association of Disabled

Madrasa Early Childhood Programme

EENET Enabling Education Network

Inclusive Learning Approach

[Maelezo ya picha: Picha iliyopo katika jalada inaonesha kundi  wamekaa katika viti  katika umbo la mduara, pembeni karibu na ukuta wamekaa viziwi wawili mbee yao yupo mkalimani anawatafsiriwa viziwi hao maneno yanaoyesemwa na mkufunzi. Mkufunzi wa kike amesimama pembeni kulia kwa mshriki ambae ni kiziwi na amevaa kanzu nyeupe. Washiriki wengine wanawake na wanaume wanamsikiliza kwa makini mkufunzi wao. ]

Unaruhusiwa kusambaza na kusanifu muongozo huu ili uendane na mazingira uliopo Hata hivyo unapaswa kutoa utambulisho sahihi, chimbuko la idhini, na uoneshe iwapo kuna mabadiliko uliyoyafanya. Unaweza kufanya hivyo kwa namna yoyote inayokubalika, lakini bila kuonesha kuwa mabadiliko au matumizi hayo yamethibitishwa na taasisi inayohodhi haki ya muongozo huu. Huruhusiwi kutumia kitabu hiki kwa lengo la kujinufaisha kibiashara. Iwapo utakihariri kijitabu hiki, kurekebisha, au kuongezea kilichoandikwa humu, utakakipokisambaza unapaswa kutumia idhini halisi kama iliyotumika kabla ya kijitabu kufanyiwa marekebisho Huruhusiwi kutumia kanuni za kisheria au teknolojia ambayo kisheria itawazuia wengine kufanya chochote katika muongozo huu ambacho idhini ya awali imeruhusu. Kwa taarifa zaidi, rejea kwenye kiungo kifuatacho: https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/legalcode

Miongozo hii inapatikana chini ya Leseni ya Creative Commons Non-Commercial

# Yaliyomo


Kipindi 0: Kutambulishana ........ 5

Kipindi cha 1: Kujuana na washiriki wengine ........ 7

Kipindi cha 2 Tunajifunza vipi? ........ 11

Kipindi cha 3: Ubaguzi ........ 20

Kipindi cha 4: Mfumo wa elimu ni nini? ........ 32

Kipindi cha 5: Elimu mjumuisho ni nini? ........ 35

Kipindi cha 6: Vikwazo vya ujumuishaji katika elimu ........ 49

Kipindi cha 7: Utetezi wa elimu mjumuisho ........ 54

Kipindi cha 8: Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho katika jamii ........ 63

Kipindi cha 9: Kutafakari kuhus kujifunza na uzowefu ........ 75

Kipindi cha 10: Kujenga Uwezo wa Utetezi: kukusanya taarifa kwa ajili ya kujenga uwelewa ........ 79

Vielelezo na vitini

Kielelezo 2.1: Kujifunza kunaonekanaje? ........ 89

Kielelezo 3.2a: Mzunguko wa ubaguzi ........ 98

Kielelezo 4.1: (a) Vipengele vya mfumo wa elimu ........ 101

Kielelezo 4.1: (b) Vipengele vya mfumo wa elimu ........ 106

Kielelezo 4.1: (c) Kuunganisha na sekta nyengine ........ 107

Kielelezo 5.2: ‘changamoto’ za mfumo wa elimu ........ 108

Kielelezo 6.2: Kutumia picha kutafakari elimu mjumuisho ........ 113

Kitini 7.2: Kushughulikia changamoto za vikwazo katika elimu mjumuisho kupitia igizo-dhima ........ 120

Kielelezo 8.1: Vichwa vya habari vya magazeti ........ 122

Kielelezo 10.2: Fomu ya hatua (Hatua zilizokubaliwa) ........ 123

# Utangulizi

Madhumuni ya mafunzo haya ni kuitambulisha elimu mjumuisho kwa wanachama wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu. Maudhui ya mafunzo haya yanatokana na moduli ya 'Utangulizi wa Elimu Mjumuisho kwa walimu', pamoja na mambo mengine yaliyoongezwa kwa ajili ya Jumuiya za Watu wenye Ulemavu.

Mafunzo haya pia yanalenga kuhusu ujuzi wa kufanya utetezi na njia bora ambazo washiriki wanaweza kuzitumia kufanya utetezi wa elimu mjumuisho katika jamii zao. Mafunzo haya yanatoa fursa kwa washiriki kujifunza kwa vitendo kwa kujifunza **zaidi kuhusu mitazamo** ya elimu mjumuisho na baadaye kutumia utafiti tatuzi kukusanya taarifa kuhusu kitu gani watu wanajua na wanafikiria kuhusu elimu mjumuisho.

Mafunzo haya ni sehemu ya mchakato wa muda mrefu wa kuzijengea uwezo Jumuiya za Watu wenye Ulemavu na mafunzo zaidi yatatayarishwa ambayo yataongezea nguvu mafunzo haya.

Mwisho wa mafunzo haya washiriki wataimarisha uwelewa wao kuhusu ujumuishaji na wataweza kuanza kufanya utetezi wa elimu mjumuisho katika jamii zao.

# Kipindi 0: Kutambulishana

## Maelekezo

- Mkaribishe kila mmoja na elezea kwanini tuko hapa kwa kutumia nukta zilizopo katika 'utangulizi' hapo juu.
- Waambie washiriki kwamba haya si mafunzo ya mara moja tu bali moduli nyengine zaidi zitatolewa ili kuongezea nguvu moduli hii.
- Elezea kuhusu walimu katika skuli za majaribio katika wilaya zao wanvyopatiwa mafunzo ya elimu mjumuisho.
- Cheza video ya Karibu katika moduli ya utangulizi wa elimu mjumuisho kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu

**Kielelezo** **Video ya makaribisho**

- Onesha slaidi ya 1 ya Pawapointi ya 'Kipindi cha Kutambulishana'. Tambulisha maudhui ya warsha.

**PawaPointi** **PawaPointi 'Utangulizi wa Vipindi vya Siku ya kwanza'**

- Onesha slaidi ya 3-4 na elezea njia za ufundishaji zitakazotumika katika warsha. Elezea kwamba tunaionesha elimu mjumuisho kwa vitendo kupitia matumizi yan jia jumuishi kama sehemu ya mafunzo. Njia hizo ni pamoja na kazi za vikundi, kazi za jozi, na fursa kadhaa za kubadilishana mawazo na uzoefu.
- Onesha slaidi ya 5-6. Eleza kwamba elimu mjumuisho inahusu kuhakikisha kwamba watoto wote waweze kuwepo skuli, kushiriki na kupata mafanikio. Onesha na jadili kuhusu picha.
- Onesha slaidi ya 7. Waambie washiriki kuhusu umuhimu wa kuwa salama wakati wa UVIKO-19. Waulize washiriki iwapo wanaweza kuongeza kitu katika orodha ya kanuni za usalama zinazohusu UVIKO-19 na uandike mawazo yao katika flipchati. Yaandike mawazo yao kwa ufupi na kwa lugha nyepesi. Yafuatayo ni maoni ya ziada ambayo yanaweza kusaidia:
    - ü **Kosha mikono kwa maji au tumia vitakasa mikono** ( sanitaiza) baada ya kugusa vitu vilivyoguswa na watu wengine.
    - ü Tumia barakoa na weka nafasi baina ya mtu na mtu kwa muda wote
    - ü Kaa karibu na meza na **uache nafasi** baina ya mtu mmoja na mwengine

- ü Mshiriki mmoja tu katika kila kikundi ashike / agawe vitini/ kadi kwa ajili ya shughuli za vikundi.
- ü Mtu mmoja tu katika kila kikundi akamate vifaa, karatasi, kalamu/penseli, gundi, wakati wa kuandika/kuonesha nukta za majadiliano na kutoa mrejesho.
- ü Wakati wa mapumziko ya chai na chakula cha mchana, **washiriki waende kwa zamu** kuchukua chakula/vinywaji na kurudi katika sehemu zao na kukaa kwa kuweka nafasi baina ya mtu mmoja na mwengine.
- ü Ikiwa hujiskii vizuri, muarifu hilo mwezeshaji/kiongozi haraka iwezekanavyo.

- Onesha slaidi ya 8. Pitia kanuni nyengine ili kufanya warsha iwe na mafanikio. Pia waulize washiriki iwapo wanataka kuongezea chochote katika kanuni hizo.
- Pitia ujuzi/stadi za mawasiliano ambazo washiriki wazifuate. Zingatia zaidi kuhusu kuwasiliana na washiriki wenye ulemavu wa uoni au usikivu waliopo katika warsha. Unaweza pia kuwataka watoe maoni yao kuhusu nini kifanyike ili washirikishwe vizuri katika mazungumzo au majadiliano.

# Kipindi cha 1: Kujuana na washiriki wengine

**Ujumbe muhimu**

Warsha ya elimu mjumuisho yenye ufanisi inahitaji washiriki kushiriki kikamilifu, wazungumze na kubadilishana mawazo.

## Maelezo kwa mwezeshaji

Mara nyingi washiriki wanafika katika mafunzo wakiwa hawajuwani. Mafunzo ya elimu mjumuisho yenye kufanikiwa, yanahitaji washiriki kuchangamka, wazungumze na kubadilishana uzowefu. Kwa hivyo, kazi ya kwanza ya mwezeshaji iwe ni kuwaongoza washiriki kujuana ili wawe huru kuzungumza. Hali hiyo itawawezesha kubadilishana maarifa, uzowefu na matarajio yao katika warsha

Kabla ya kuanza shughuli ya pili katika kipindi hiki unahitaji kutayarisha mchoro wa **‘ Mto wa Maisha’**. Katika kutayarisha mto wa maisha chukua karatasi za flipchati (kiasi 6 au 8) na uziunganishe pamoja ili upate nafasi kubwa ya kuchorea mto wa maisha utakaoonekana vizuri na washiriki wote. Chora mto huo katika hizo karatasi za flipchati na uzibandike ukutani.

**Katika kipindi hiki washiriki:**

- ü Watabadilishana uzowefu wao katika masuala ya elimu mjumuisho
- ü Watasema kuhusu matarajio yao katika mafunzo
- ü Wataanza kuwajua washiriki wenzao katika warsha

## Shughuli 1.1: Mchezo wa kujuana

1 Dakika 20

## Maelekezo

- Mpe kila mshiriki kadi mbili za karatasi zenye rangi tofauti. Ikiwa kuna washirki wenye uoni hafifu ni bora kutumia karatasi kubwa kuliko kadi.
- Onesha Pawapointi “ Kipindi cha 1: Kujuana’ slaidi ya 1.

**PawaPointi** **Pawapointi “ Kipindi cha 1: Kujuana’ slaidi ya 1.**

- Watake washiriki waandike na kukamilisha kauli zifuatazo, moja katika kila kadi/ karatasi. Iwapo wanapata shida ya kuandika wanaweza kumwomba mtu mwengine kuwasaidia.

.... Kuhusiana na elimu mjumuisho naweza kusaidia .....

Kuhusiana na elimu mjumuisho ningependa kufahamu ....

- Kila mshiriki aandike kila kauli katika kadi yenye rangi moja, kwa mfano kauli ya kwanza iandikwe katika rangi ya manjano na washiriki wote , na ya pili iandikwe katika rangi ya machungwa na washiriki wote.
- Baadae washiriki watajiwekea kadi hizo katika miili yao, mfano, mabegani, au kunyanyua juu kadi zao huku wakizunguka darasani kutafuta na kuzungumza na watu ambao kadi zao zimefanana. Kwa mfano watapaswa kutafuta mtu ambae anayo taaluma ya jambo wanalohitaji kulielewa.
- Unaweza kuhitaji kuwasaidia watu wachache 'kutafuta wanaolingana nao', ikiwa washiriki wameonesha ugumu tangu mapema hawafahamu nini wafanye; mwisho wa "Mchezo wa Kujuana" mkufunzi anaweza kuwataka washiriki wachache kujitolea kuwaeleza wenzao ni kipi wameoanisha na wenzao na yepi wamejadili.
- Mwisho washiriki wa mchezo wa kujuana watawauliza baadhi ya washiriki watakaopenda kuwaambia washriki wengine kuhusu watu waliojuana nao na nini walikijadili.



Washiriki wakiwa katika mchezo wa kujuana nchini Zanzibar

[Maelezo ya picha: Watu wazima wawili wanaume wakiwa mbele wameelekeana. Kuna watu wengine wawili wakionekana kufanya hivyo hivyo. Watu wanatizamana na kuzungumngumza wakiwa wameelekeana.]

## Shughuli 1.2: Mto wa Maisha

1 Dakika 30–45

### Maelekezo


- Washiriki wakae katika vikundi vidogo vidogo wakiwa na karatasi, penseli, penseli za rangi, na mikasi.
- Onesha Pawapointi 'Kipindi cha 1: Kujuana' slaidi ya 2 kisha pitia dhamana na majukumu ya kila mmoja katika kazi za vikundi ikiwemo kanuni za usalama za UVIKO-19 kabla ya kuanza shughuli.

**PawaPointi** **PawaPointi ya 'Kipindi cha 1: Kujuana'**

- Watake washiriki waangalie katika ' Mto wa maisha' ukutani. Waeleze washiriki kwamba sehemu tofauti za mto huu zinawakilisha nyakati tofauti:
  - o robo ya kwanza ya mto kutoka juu = wakati uliopo
  - o robo mbili za katikati = wakati wa sasa na wakati wa warsha hii
  - o robo ya mwisho= wakati ujao
- Elezea kwamba mto unaelezea mzunguko wa maisha yetu kutoka wakati uliopita (uzowefu tunaoleta katika warsha), kupitia wakati uliopo ( hapa tulipo sasa), hadi wakati ujao ( tutakachojifunza katika warsha, kitu gani tunatarajia kujifunza, na kitu gani tunatarajia kuanza kufanya).
- Watake washiriki wachore picha inayowakilisha uzowefu wa wa masuala ya elimu, na waoneshe picha hizo katika vikundi vyao. Inaweza kuwa uzowefu binafsi wa washiriki wakati walipokuwa skuli au uzowefu wao kama watu wazima.
- Katika vikundi vyao waulizane kuhusu picha zao na hii itawasaidia kujitambulisha na kujuana vizuri zaidi.
- Waambie washiriki wakate picha hizo na waziweke katika robo ya Mto wa Maisha, kuandika uzowefu wao wa wakati uliopita. Mwezeshaji, anaweza

kuchagua baadhi ya picha na kuwataka washiriki kutoa maelezo ya baadhi ya picha.

- **Kwa kuongezea, washiriki wanaweza kubandika kadi zao za ' Kuhusu elimu mjumuisho Ninajua/ naweza kuelezea...'** mwanzo wa mto wa maisha, kama inavyooneshwa katika mchoro ufuatao.
- Kisha wape kila washirki 3 kadi ambazo wazitumie kuandika **matokeo matatu au maswali** matatu kuhusu elimu mjumuisho ambayo wanataka yajibiwe katika warsha hii. Moja kati ya kadi hizi inaweza kuwa ni ile ya ' Ningependa kujua...' kutoka katika Shughuli ya 1.
- Watake washiriki wabandike kadi hizi tatu mwanzoni mwa robo ya pili ya mto (ukiwakilisha mwanzo wa warsha).
- Katika wakati ufuatao wa mapumziko, wewe pamoja na/au baadhi ya washiriki wanaweza kupanga upya kadi katika makundi yenye mambo au maswali yaliyofanana.



Mfano wa Mto wa Maisha uliochorwa na washiriki nchini Zanzibar

[Maelezo ya picha: Mchoro wa mstari unaoonesha mto wa maisha au njia unaopita kwa mlalo katikati ya karatasi kubwa. Kadi zenye gundi zimebandikwa upande wa kushoto wa karatasi hiyo.]

# Kipindi cha 2 Tunajifunza vipi?

**Ujumbe muhimu**

Kujifunza kunatokea kila pahala, kila wakati. Kujifunza hakutokei skuli tu. Kuna fursa nyingi za kujifunza nyumbani na katika jamii na fursa hizi huendelea katika maisha yetu yote.

## Maelezo ya mwezeshaji

- Kabla ya kuanza kufikiria kuhusu elimu mjumuisho, ni muhimu kufikiria namna tunavyojifunza—tukiwa watoto na pia tukiwa watu wazima. Kuelewa njia mbalimbali za kujifunza namna zinavyotokea kutatusaidia kuweza kusaidia vizuri zaidi njia ya elimu mjumuisho ya kujifunza kuanzia nyumbani, skuli na katika jamii.
- Kucheza ni chanzo muhimu cha kujifunza kwa watoto wote na sio kwa w.atoto wadogo pekee. Tunapocheza, tunafanya majaribio, tunabuni na kutumia stadi za utatuzi-wa matatizo ambapo zote hizo ni stadi muhimu za kujifunza
- Watoto pia hujifunza kupitia kusaidia kazi za nyumbani na kupitia kushirikishwa katika shughuli za kila siku kama vile kupika, na kupanda mimea ya chakula na hizi zote ni stadi muhimu katika maisha. Huhitaji nyenzo mahsusi kwa ajili ya kusaidia kujifunza nyumbani, kila siku vitu unavyovikuta maeneo ya nyumbani vinaweza kusaidia katika kujifunza.
- Skuli zinazingatia kujifunza taaluma ingawaje maeneo mengine ya ujifunzaji na ukuaji ni muhimu pia; maeneo haya ni pamoja na stadi za kijamii, ustawi wa kimaono, uratibu wa viungo, ubunifu na imani ya kidini. Njia nzuri ya kukumbuka baadhi ya maeneo muhimu ya ukuaji wa mtoto ni KI4 **Kijamii, Kimwili, Kiakili, Kibunifu, Kihisia na kiimani.**
- Njia nyingi za kuunga mkono ujifunzaji kwa watoto pia zinafaa kwa watu wazima. Hata hivyo, watu wazima pia wana uzowefu wa kimaisha na kwa hivyo tunaweka msisitizo zaidi kwa baadhi ya shughuli ambazo watu wazima hujifunza wakati wa warsha za mafunzo kama hizi, ikiwa ni pamoja na kubadilishana uzowefu, kutatua matatizo kwa pamoja, huku wakitumia uzowefu wao katika maisha halisi au katika kazi zao na kuelewa kwa nini jambo fulani ni muhimu.

**Katika kipindi hiki washiriki:**

ü Watafikiria njia mbalimbali za kujifunza na jukumu ambalo wazazi, walezi na wanajamii wanaweza kuchukua katika kuunga mkono ujifunzaji.

ü Kutafakari katika uzowefu wako mwenyewe wa kujifunza.

ü Kutafakari shughuli mbalimbali za kuunga mkono kujifunza kwa watoto na watu wazima.

## Shughuli 2.1: Je kujifunza ni nini?

1 Dakika 30

**Kielelezo 2.1** **Picha za watu wakifanya shughuli mbalimbali**

### Maelekezo

- Toa seti moja kamili ya picha kwa kila kikundi. Kuna picha 8 katika seti hiyo na zinapatikana mwishoni mwa muongozo huu wa mwezeshaji (mfano mmoja unaoneshwa hapa chini).
- Waambie washiriki kwamba picha zote zinaonesha watu wakiwa peke yao au wakiwa na watu wengine wakifanya shughuli mbalimbali.



[Maelezo ya picha: Bibi kizee amekaa katika kitimwendo. Anazungumza kwa ishara kwa kutumia mikono. Viduara vya mazungumzo vinaonesha kwamba anasimulia hadithi au kuelezea ndoto fulani. Katika kiduara cha mazungumzo mtu mmoja anayeonekana kama bibi kizee amelala. Mtu huyo anaota kwamba anaruka angani. Kikundi cha watu wazima na watoto wa umri mbalimbali, ikiwa ni pamoja na mtoto mmoja mwenye ualblino, wamekaa sakafuni. Nyuso zao zinaonesha kuwa wanamsikiliza bibi kizee kwa makini.]

**PawaPointi** **PawaPointi 'Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza**

- Onesha Pawapointi ya **'Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza'** na watake washiriki wajadili maswali yafuatayo katika slaidi ya 1 katika vikundi vyao.
  - Picha zipi zinaonesha mifano ya namna kujifunza kunavyotokea?
  - Picha zipi hazinaoneshi mifano ya namna kujifunza kunavyotokea?
  - Kwa kila picha elezea ni wapi unadhani kujifunza kunatokea , je, unaweza kuelezea ni ujifunzaji gani unaotokea?
  - Itasaidia kuonesha mfano mmoja kwa washiriki wote kwa kutumia mfano mmoja katika sehemu ya vielelezo iliyopo mwishoni mwa muongozo huu.
- Inaweza kuwa ni wazo zuri kuwataka washiriki kufikiria kujifunza mambo ya kiimani na wachore mchoro unaoonesha hivyo. ( kwa mfano wanaweza kuchora mchoro wa mtoto anayesoma Qur'an au mtoto anayeswali au mtoto anayemshika mkono mwenziwe mdogo na mchoro wa kiduara kinachooonesha ' Allah anawapenda watu wanaosaidia wenzao')
- Baada ya kila kikundi kujadili picha zote, watake washiriki wa kila kikundi kuwasilisha kazi zao kwa washiriki wote kwa zamu. Baada ya kikundi kimoja kuwasilisha kazi yake watake washiriki wengine kuongeza mawazo yao juu ya mchoro uliowasilishwa, kabla ya kuendelea na kikundi kinachofuata kuonesha mchoro wao.

Maelezo kwa mwezeshaji: Kujifunza kunatokea katika kila mchoro. Hata hivyo vikundi vinaweza kuwa na maoni tofauti kuhusu aina mbalimbali za kujifunza zinavyotokea. Hakuna jawabu sahihi na isiyo sahihi. Chini ya kila picha katika sehemu ya vielelezo utaona maelezo kuhusu aina za kujifunza ambazo washiriki wanaweza kuzitaja na hivyo unaweza kuzitumia pia kwa washiriki wote.

- Taja nukta zifuatazo wakati wa mjadala kwa washirik wote, si lazima kuzitaja kwa mpangilio maalum:
  - ü Kucheza ni chanzo muhimu cha kujifunza kwa watoto wote na sio kwa watoto wadogo tu. Tunapocheza, tunafanya majaribio na tunatumia stadi za utatuzi wa matatizo ambazo pia ni miongoni mwa stadi muhimu za kujifunza
  - ü Watoto pia hujifunza kwa kusaidia kazi za nyumbani na kupitia kushirikishwa katika shughuli za kila siku kama vile kupika, kupanda mimea ya chakula na zote hizi ni stadi muhimu za maisha
  - ü Kujifunza hakutokei katika skuli tu. Kuna fursa nyingi za kujifunza nyumbani na katika jamii na fursa hizi huendelea katika maisha yetu yote. Kujifunza kunatokea kila pahala, kila wakati.
  - ü Huhitaji nyenzo mahsusi kwa ajili ya kusaidia kujifunza nyumbani, kila siku vitu unavyovikuta maeneo ya nyumbani vinaweza kusaidia katika kujifunza.
  - ü Skuli zinazingatia kujifunza taaluma ingawaje maeneo mengine ya ujifunzaji na ukuaji ni muhimu pia; maeneo haya ni pamoja na stadi za kijamii, ustawi wa kimaono, uratibu wa viungo, ubunifu na imani ya kidini. Maeneo yote haya yanaungana pamoja kutoa msingi imara katika kujifunza.
- Onesha Pawapointi ya Kipindi cha 2 slaidi ya 2 ' Namna Tunavyojifunza' ili kueleza kwa ufupi nukta muhimu.

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 2: 'Namna tunavyojifunza'**

## Shughuli ya 2.2: Wakati gani nilihangaika kujifunza jambo jipya, na kitu gani kilinisaidia? (shughuli ya ziada)

1 Dakika 30 au zaidi

Katika shughuli hii, washiriki watazingatia uzowefu wao wa kujifunza katika maisha yao ya kila siku.

Hii ni 'shughuli ya ziada'. Ikiwa unadhani huna muda wa kuingiza shughuli hii, unaweza kuiacha.

### Maelekezo

- Onesha Pawapointi ya Kipindi cha 2 'jinsi tunavyojifunza' slaidi ya tatu.

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 2: 'Namna tunavyojifunza'**

- Kwanza, kila mshiriki atachora picha isiyokuwa na maelezo, kuonesha matukio katika maisha yao wakati walipokuwa wakijaribu kujifunza mambo fulani, lakini wakapata ugumu wa kufanikiwa. Kwa mfano, kujitahidi kusoma wakiwa skuli (kama; kjifunza hesabu mpya). Au nyumbani (kujaribu kushona viatu) Au wakati wa utu uzima, (kujifunza lugha nyengine).
- Unaweza kuonesha shughuli hii kwa kuanza wewe kuchora kitu ambacho wewe mwenyewe ulijifunza na kisha uwatake washiriki kufikiria hali ilivyokuwa.
- Baadae watakaa kwa jozi. Mshiriki mmoja atamtizama mwenzake akichora na kujaribu kukisia hali ilivyokuwa. Ikiwa watashindwa kukisia, mwenzake anayechora anaweza kumueleza mwenzake kuhusu jinsi walivyosumbuka kujifunza. Maswali yafuatayo yatapaswa kutumika kuongoza mjadala juu ya mchoro huo/ hali hiyo:
  - Ni mbinu zipi zilitumika kukufundisha?
  - Je, kuna mtu yeyote aliyejaribu kukusaidia kujifunza? Kama ndiyo, ni akina nani hao? Msaada wao ulifaa?
  - Jambo gani jengine ambalo unahisi kama lingefanyika lingekusaidia kujifunza kwa haraka na ufanisi?

- Baadae washiriki watabadilishana na mtu mwengine atamueleza mwenzake historia yake na kuyajibu maswali hayo.
- Baada ya jozi zote kumaliza mijadala yao juu ya picha walizochora, mkufunzi anaweza kuendesha mjadala mfupi kuhusiana na:
  - Ni vipi vikwazo vya kujifunza ambavyo washiriki walikumbana navyo?
  - Ni kitu gani na nani aliwasaidia wakati walipopata changamoto?

**PawaPointi** **PawaPointi 'Kipindi cha 2: namna tunavyojifunza'**

- Onesha PawaPointi ya 2 ' Namna tunavyojifunza' slaidi ya 4 na elezea nukta ifuatayo:

Tunajifunza mambo kwa sababu tunataka au tunahitaji, tunajifunza kwa **kutenda**, **kwa kufanya mazoezi** na kwa **kupata usaidizi**. Hii ni kweli kwa watoto na watu wazima.

## Shughuli ya 2.3: Video ya ufundishaji na ujfunzaji jumuishi

### Maelezo ya mwezeshaji

- Ufundishaji katika skuli mara nyingi humzingatia sana mwalimu ambapo mwalimu huonekana ' ni chanzo cha maarifa yote'
- Hatahivyo, Ushahidi umeonesha ni jinsi gani **njia za ujifunzaji unaomzingatia mwanafunzi**, zilivyo muhimu katika kuwawzesha wanafunzi kutumia zana na mazingira yao katika njia shirikishi zaidi.
- Mhamo kuelekea matumizi ya njia hizi unaweza kuonekana katika nchi nyingi, hata kama bado hazijatekelezwa kikamilifu.
- Walimu wanaendelea kushajiishwa kutumia njia na mikakati shirikishi zaidi ya kufundishia na kujifunzia darasani.
- Kwa upande wa wanafunzi, sasa hawaonekani tena kuwa ni wapokeaji tu wa ujifunzaji bali wanatakiwa kuwa 'hai' katika mchakato wa kujifunza. Wanatarajiwa **kuuliza maswali, kufikiria mawazo mapya, kuvumbua, kushirikiana na wengine na kutatua matatizo**.

- Katkika kuunga mkono hili, walimu wanashajiishwa kutumia  darasani shughuli  zinazohusisha usimuliaji wa hadithi, igizo-dhima, kazi za vikundi na ujifunzaji unaoakisi maisha halisi.

1 Dakika 45 au zaidi

- Waambie washiriki kwamba wataangalia video ya walimu katika nchi mbalimbali zenye kipato cha chini wakitumia shughuli mbalimbali katika kusaidia ujifunzaji wakati wa ufundishaji wao.
- Video hii ni miongoni mwa  mlolongo wa video ambazo jumuiya ya EENET ilitoa. Video hiyo inaitwa ‘ Siku Jumuishi’. Kuna video hizo 10 kwa jumla. Video hii ni nambari 7 ambayo inaitwa ‘Kufundisha na Kujifunza’. Video hii inachukua dakika 10.
- Wakati washiriki wakiwa wanaangalia, watake wafikirie kuhusu swali lifuatalo:

**Ni njia zipi  wanazotumia walimu kuuunga mkono kujifunza?**

- Chezesha video ya ‘ Siku Jumuishi Programu nambari 7: ‘Kufundisha na Kujifunza’

**Kielelezo** **Video: ‘Siku Jumuishi Programu ya 7: ‘Kufundisha na Kujifunza’**

- Hakikisha unaisimamisha video ifikapo dakika 09:55 baada ya mwalimu kusema, ‘watoto ni watendaji wakuu katika elimu yao’.
- Onesha PawaPointi ‘Kipindi cha 2: ‘Namna tunavyojifunza’ slaidi ya 5

**PawaPointi** **PawaPointi ‘‘Kipindi cha 2: ‘Namna tunavyojifunza’**

- Baada ya kuangalia, watake washiriki wakae katika vikundi vidogo vidogo kujadili swali na waandike njia mbalimbali za kuunga mkono kujifunza ambazo wameziona
- Watake washiriki watoe mrejesho kwa pamoja na nakili mawazo yao katika flipchati

- Ifuatayo ni orodha kamili ya shughuli na njia zinazoonekana katika video. Hatahivyo, usitarajie washiriki kutaja kila kitu katika orodha hiyo au kutumia maneno kama yalivyo katika orodha

Hii hapa orodha kamili ya njia zilizoonekana katika video:

- Shuguli zinazohusisha kutizama/kuangalia
- Shughuli zinazohusisha kusikiliza na kuelewa
- Shughuli zinazohusisha kuzungumza
- Shughuli zinazohusisha kugusa
- Shughuli zinazohusisha kutembea
- Kutumia michezo
- Kutumia wanaserere/ vifaa vya kuchezea
- Kufanya masomo yawiane na uzowefu katika maisha halisi
- Kutumia vitu/ mazingira halisi na vitu vilivyotengenezwa upya kwa kutumia vitu vilivyokwishatumika
- Kutumia igizo-dhima, tamthilia na uigizaji
- Kutumia maeneo ya nje ya jengo
- Kufanya kazi kwa vikundi
- Kufanya kazi kwa jozi

- Waulize washiriki: **Kwa nini ni muhimu kuelewa zaidi kuhusu namna tunavyojifunza kwa ajili ya elimu mjumuisho?**

**PawaPointi** **PawaPointi 'Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza'**

- Onesha slaidi ya 6 kutoka PawaPointi ya Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza
- Elezea yafuatayo, **kuelewa zaidi kuhusu namna tunavyojifunza** ni muhimu kwa sababu inasaidia:
  - ü Walimu wanafikiria namna bora zaidi ya kuunga mkono kujifunza darasani na skuli

- ambazo zinahusisha kutumia shughuli shirikishi na zenye kujenga ubunifu darasani, kama vile kufanyakazi kwa vikundi, kutatua matatizo na kutumia hadithi na mawazo mbalimbali

ü Wazazi na walezi wanafikiria kuhusu namna bora ya kuunga mkono ujifunzaji nyumbani na katika jamii

- Ujifunzaji unaohusisha kujenga fursa za kujifunza nyumbani kupitia shughuli za kila siku, kama vile kupika, kupanda mimea ya chakula, na kujifunza stadi mpya kutoka kwa watu mbalimbali katika familia na jamii.

· Eleza kwamba njia nyingi za kuunga mkono ujifunzaji zinafaa kwa wote, watoto na watu wazima.

· Kuna kitu muhimu ambacho watu wazima wanacho lakini watoto hawana – **Uzowefu wa kimaisha**

**PawaPointi**

**PawaPointi 'Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza'**

· Onesha slaidi ya 7 kutoka **PawaPointi 'Kipindi cha 2: Namna tunavyojifunza'.**

· Hii ina maana kwamba tunaweka msisitizo wa ziada katika baadhi ya shughuli ambazo zinawasaidia watu wazima kujifunza katika warsha kama hizi. Hizi ni pamoja na

ü ... kubadilishana uzowefu

ü ... kutatua matatizo kwa pamoja

ü ... kutumia ujifunzaji wao katika maisha halisi au makazini mwao

ü ... kuelewa kwa nini kitu fulani ni muhimu

· Waambie washiriki kwamba watu wazima wanajifunza vizuri zaidi wanapo fanya shughuli zote zilizotajwa hapa. Kwa hivyo, tutakuwa tukitumia aina nyingi ya shughuli hizo katika mafunzo haya.

# Kipindi cha 3: Ubaguzi

**Ujumbe muhimu**

Tunapoelewa zaidi kuhusu mizizi ya ubaguzi, tutakuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuukomesha ubaguzi— kwa mtu yeyote au kikundi chochote. Hii inamaana ya kuwa kunaweza kuwa jumuishi- kwa mtu yeyote au kikundi.

## Maelezo ya mwezeshaji

- Sote tunahitaji kutafakari juu ya maana ya ubaguzi, chanzo chake, na vipi sote tunaweza kusaidia kuukomesha.
- Ni muhimu sana sana sote kuwa na uelewa mpana zaidi kuhusu ubaguzi katika jamii. Ubaguzi dhidi ya wanawake, dhidi ya watu wenye ulemavu na au mahitaji maalum, dhidi ya lugha, kabila au dini ya watu wachache, dhidi ya wahamiaji na kadhalika.
- Katika mafunzo kwa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu ni vigumu kwa washiriki kuepuka kujikita zaidi katika kuzuungumzia ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu.Hatahivyo, ni muhimu kwa mwezeshaji kujaribu kupanua majadiliano kuingiza maeneo mengine ya ubaguzi, ikiwa ni pamoja na jinsia, lugha, makabila ya wachache, na maeneo mengine yanayofaa katika mazingira husika.
- Kama tunaelewa zaidi kuhusu mizizi ya ubaguzi, tunaweza kuwa na uwezo mkubwa wa kuukomesha –kwa mtu yoyote au kundi lolote.

### Katika kipindi hiki washiriki:

ü Wataangalia kwa undani maana ya ubaguzi

ü Wataangalia kwa undani chanzo cha ubaguzi

ü Watajadili njia za kukomesha ubaguzi


## Activity 3.1: Kufafanua Ubaguzi

1 Dakika 30

### Maelekezo

- Ask participants to work in small groups and give each group a piece of flipchart paper. At the top is written: “Discrimination means…”. Watake washiriki wafanye kazi katika vikundi vidogo vidogo na wape kila kikundi karatasi ya flipchati. Juu iwe imeandikwa: “Ubaguzi ni.....”
- Nyanyua kikaratasi na uwaonyeshe washiriki jinsi ya kukunja hio karatasi ili kila mstari ufichike. Wape vikundi maelekezo yafuatayo:


  “Mtu mmoja katika kikundi chako aandike katika mstari mmoja “maana ya ubaguzi”. Waandike ufafanuzi huo bila ya watu wengine katika kikundi kuona kilichoandikwa. Baadae wazikunje karatasi zao kiasi kwamba ufafanuzi wao hauonekani kisha karatasi yake ampe mwenzake. Zoezi hili liendelee hadi kila mtu katika kikundi amepata nafasi ya kuandika japo mstari mmoja wa maana ya ubaguzi. Unaweza ukavipitia vikundi wakati zoezi likiendelea.”




Kunja karatasi kiasi ambacho anayeandika atauona mstari wake tu na sio kuona yaliyoandikwa na wenzake.

[Maelezo ya picha: Karatasi ilioandikwa juu ‘ubaguzi unamaanisha....’,na wazo moja lilioandikwa chini yake.]

- Baada ya dakika 10, mwezeshaji atake kila kikundi kukunjua karatasi zao na kwa pamoja wasome mistari inayoelezea maana ya ubaguzi.




Mfano wa karatasi iliyokunjuliwa ikionesha maelezo walioyaandika

[Maelezo ya picha: karatasi ikionesha maelezo tafauti ya washiriki katika kikundi.]

**PawaPointi** **PawaPointi ya Kipindi cha 3 ‘Ubaguzi’**

- Sasa vitake vikundi kujadiliana maswali yafuatayo:
  - Je, ufafanuzi wenu umefanana au umetafautiana? Kivipi?
  - Je, kuna ufafanuzi wowote ambao hamkubaliani nao?
  - Hivi sasa mmeshaona ufafanuzi wa kila mmoja, je, kuna lolote mngetaka kuongezea?
  - Katika vikundi vyenu, tumieni mawazo mlioyaandika kujadiliana hadi mpate ufafanuzi mmoja tu juu ya ubaguzi ambao mtakubaliana nao.

- Baada ya dakika 10 vitake vikundi kuwasilisha ufafanuzi wao mfupi kwa washiriki wote. Andika kila ufafanuzi katika flipchati kisha uwaoneshe ufafanuzi ufuatao wa ubaguzi katika kipindi cha tatu cha pawapointi:

| |
|---|
| Ubaguzi ni kitendo cha kulinyima kundi fulani la watu kupata haki na nyenzo kwa msingi wa usawa |

- Mwisho, watake washiriki wajadili kwa ufupi kuhusu ufafanuzi huu na waulinganishe na ufafanuzi uliotolewa na washiriki.

## Shughuli ya 3.2: Chanzo cha ubaguzi ni nini? Kwa nini ubaguzi unatokea?

1 Dakika 60

**Maelekezo:**

- Fafanua kuwa sote tunaweza kuwa na uzowefu mbalimbali kuhusu ubaguzi. Uzowefu huo unaweza kuwa tofauti hata kama sote tunatokea katika kijiji kimoja, dini moja au hata familia moja.
- Tabia ya kibaguzi inaanzia kutoka namna watu wanavyowasiliana, wakitengana katika mazungumzo hadi katika unyanyasaji wa kimwili na hata unyanyasaji unaoandaliwa.
- Sisitiza umuhimu wa kila mmoja kuhisi amejumuishwa katika shughuli inayofuata.
- Sisitiza umuhimu wa kusikiliza na kuheshimu uzowefu wa kila mmoja na kutambua mchango wa kila mmoja kwa viwango tofauti na ujuzi tofauti ambapo mara nyingi ni kwa sabau baadhi ya watu walipata fursa zaidi za kielimu kuliko wengine.

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 3 'Ubaguzi'**

- Watake washiriki kufanyakazi kwa jozi.
- Onesha slaidi ya 5 katika Pawapointi ya Kipindi cha 3 'Ubaguzi' na toa maelekezo yafuatayo:

"Fikiria wakati wowote katika maisha yako ambao uliwahi kubaguliwa. Inaweza kuwa ulibaguliwa kwa sababu ya jinsia yako, ulemavu, umri, kabila, dini, lugha, umasikini, eneo la kijografia (kutoka mjini kwenda shamba)n.k. Mueleze mwenzio kuhusu ubaguzi huo":

- Nini kilitokea ?
- Watu wengine walisema nini au walifanya nini?
- Ulijisikiaje?

- Ulifanya nini au ulijibu nini?

- Baada ya jozi zote kuwasilisha mifano yao na kujibu maswali hayo, mkufunzi atawauliza tena swali lifuatalo:
    - Unafikiri kwa nini watu waliokufanyia ubaguzi walifanya hivyo?
- Baada ya dakika chache, watake baadhi ya washiriki wajitolee kueleza mawazo yao pamoja na darasa zima kujadili kwa nini ubaguzi hutokea. Sio lazima kwa mshiriki kutoa hadithi yote kwa darasa zima.
- Andika michango ya mijadala katika karatasi ya flipchati. Kisanduku kilichopo hapo chini kinayo baadhi ya majibu ambayo unaweza kuwapa washiriki hasa ukiona kwamba washiriki wanasumbuka kupata majibu:
-

**Kwa nini ubaguzi hutokea? Majibu ambayo unaweza kuwaongoza washiriki**

- **Inawezekana watu wasijuwe** kama wanabagua; wanaweza kudhania tabia na desturi zao ni za kawaida na zinakubalika.
- Zipo dhana nyingi katika jamii (mfano; katika jamii ipo dhana kwamba wanawake hawawezi kuendesha gari vizuri; au kwamba watoto wenye ulemavu hawawezi kujifunza taaluma). Watoto hukua huku wakisikia itikadi kama hizo kwa watu wazima (kwa mfano, wanawasikia wanaume wakifanya utani kuhusu wanawake kuendesha gari vibaya" " au kuwasikia walimu ama watu wazima wengine kuwaita watoto wenye ulemavu au mahitaji maalum ya kielimu; 'wazito' au 'wapumbavu'). Watoto huanza kuzichukulia dhana hizo kuwa ni za kweli. Kwa hiyo wanapokuwa watu wazima hujikuta wakiziendeleza dhana hizo; (Kwa mfano kukataa kukodi teksi ya dereva mwanamke eti kwa sababu atakuwa ni dereva mbaya; au kukataa kumfundisha au kumuajiri mtu mwenye ulemavu kwa kuamini kwamba hawezi kusomesheka au kuajirika). **Tabia hii inajikita katika dhana potofu ya ubaguzi.**
- Watu **huweza kubagua kwa sababu ya kuogopa.** Kwa mfano, wanaweza kuyaogopa baadhi ya makundi ya watu ambao ni hatari. (Kwa mfano kuogopa ulemavu kuwa kama ni nuksi au kuwaogopa watu kutoka katika dini fulani kwa sababu ni magaidi). Au wanaweza kuogopa kuwa kuna makundi yanakwenda kulihodhi jambo ambalo ni muhimu. (Kwa mfano kupata hofu kwamba wahamiaji watawanyang'anya kazi wenyeji. Mara nyingi woga kama huu unasababishwa na dhana potofu.

- Watu huweza kubagua ili **kudhibiti au kujijengea misingi ya nguvu**. Wanaamini kwamba wanaweza kuongeza nguvu zao kwa kunyima haki na uhuru kwa watu au makundi mengine.

- Malizia mjadala kwa kuonesha slaidi ya 6 inayoonesha **' mzunguko wa ubaguzi'**

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 3 'Ubaguzi'**

- Wasilisha kila hatua ya mzunguko. Ili kuwasilisha vizuri, unaweza kutumia muktadha wako halisi au unaweza kutumia mfano wa jinsia uliotolewa katika **Kielelezo cha 3.2b.**

  "Tunaweza kuona kutoka shughuli zilizotangulia pamoja na mijadala kwamba ubaguzi unaweza ukawa kama duara. Watoto hukuwa huku wakisikia dhana potofu, wakisikia maelezo yasio na msingi na kujionea tabia za kibaguzi miongoni mwa watu wazima. Wanadhani hii ni kawaida tu kwa hiyo na wao huendeleza tabia hizo hizo wakati wanapokuwa watu wazima. Ili kuijenga jamii yetu katika msingi wa usawa kwa wote, na kumpatia kila mmoja haki yake ya kuishi, kujifunza na kufanyakazi kwa furaha, kwa afya na uzalishaji, tunahitaji kulivunja duara hili la ubaguzi. Hii ina maana kwamba, kila mmoja wetu anapaswa kutamka kwamba: "Ubaguzi haukubaliki na nitafanya jambo lolote kuukomesha".

- Waambie washiriki kutizama **Kielelezo 3.2a na Kielelezo 3.2b** kisha wajadili katika vikundi vyao "Mzunguko wa Ubaguzi". Waambie wajadili kitu gani wanafikiri kinatokea katika picha zilizomo katika **Kielelezo 3.2b** iwapo hujaitambulisha kabla. Watake washiriki pia kufikiria jinsi wanavyoweza kuchukua hatua ili kuuvunja mzunguko unaosababisha ubaguzi.

**Kitini 3.2a na 3.2b** **Mchoro wa mzunguko wa ubaguzi**

- Sasa wape washiriki maelekezo haya(katika PawaPointi ya Kipindi cha 3: slaidi ya 7):

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 3 'Ubaguzi'**

“Fikirieni tena juu ya uzowefu wenu wa masuala ya ubaguzi. Mkae katika jozi au watu watatu watatu mjadili maswali yafuatayo:’’

- Je wewe mwenyewe au unamfahamu mtu yeyote aliyefanikiwa kukomesha vitendo vya ubaguzi? Kama ndiyo, kivipi? Nani alisaidia?
- Iwapo ubaguzi haukuweza kukomesheka, unafikiri ilikuwa nini kifanyike ili kuukomesha – na unadhani nani angesaidia hali hiyo?

- Baada ya dakika 10 watake washiriki kubadilishana mawazo yao na darasa zima kujadili kwa njia gani ubaguzi uliondoshwa au haukuweza kuondoshwa. Onesha kuridhia matokeo yoyote yaliyojitokeza.
- Andika majibu ya washiriki katika karatasi ya flipchati. Ikiwezekana majibu yaliofanana yawekwe pamoja. Tumia kalamu ya rangi tafauti kuainisha mtu aliyesaidia kukomesha ubaguzi huo.

Mifano ya baadhi ya majibu yanayofaa

- Labda kuna mtu fulani mwenye nguvu (kwa mfano; mzazi, mwalimu, kiongozi) amezungumza na watu wenye kufanya ubaguzi na wakakubali kuachana na tabia hiyo.
- Watu mbalimbali waliokuwa wakibaguliwa waliwafuata kwa pamoja watu wanaowabagua na wale watu wakaacha tabia hiyo.
- Tuliamua kuwakimbia (kwa muda au moja kwa moja)
- Tuliviripoti vitendo vyao vya ubaguzi kwenye vyombo vya sheria. (Mfano; polisi, mahkama n.k) na wahusika waliamua kuachana navyo.
- Tuliamua kupaza sauti juu ya hali hiyo mpaka hali ikafifia.
- Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa kukomesha hali hiyo.

## Shughuli ya 3.3: Mchezo wa Maisha

1 Dakika 30

### Maelekezo

- Waombe washiriki 7 wajitolee. Hamasisha kuwe na wanaume na wanawake.
- Mpe kila mmoja katika washiriki waliojitolea majukumu yafuatayo (wachukue majukumu hayo bila ya kuyaona kwanza ili wasijue mapema majukumu watakayotakiwa kuja kufanya.
- Andika kila jukumu kwa maandishi makubwa katika karatasi ya A4 kabla ya shughuli na wape karatasi hizi wale wote waliojitolea.
    - **mtoto wa kiume kutoka katika eneo la mjini lenye umasikini**
    - **mtoto wa kiume wa mwanasiasa mashuhuri katika mji wa Zanzibar**
    - **mtoto wa kiume mwenye ulemavu wa viungo na wazazi wake ni matajiri**
    - **mtoto wa kike mwenye maradhi ya ukoma anayetokea maeneo ya vijijini**
    - **mtoto wa kiume anayetokea kijijini**
    - **mtoto wa kike aliyeolewa mapema na sasa ni mjamzito**
    - **mtoto wa kike kutoka katika familia inayoishi mjini Zanzibar**
- Waambie wale washiriki 7 waliojitolea wasogee katikati ya chumba cha mafunzo na waombe washiriki waliobaki wakae upande mmoja lakini wawakabili waliojitolea na waweze kuwaona. Waliojitolea wasimame katika mstari na waache nafasi baina yao wakiwakabili washiriki waliokaa. Wanyanyue zile karatasi zilizoandikwa majukumu yao wazioneshe kwa washiriki wazione vizuri.
- Mwombe kila aliyejitolea kwa sauti kusoma kwa zamu jukumu lake.
- Elezea jinsi utakavyosimulia hadithi ya maisha, ukichukua wahusika katika safari kutoka kuzaliwa hadi uzeeni. Kila unapofika katika tukio muhimu la kimaisha, utawauliza wajibu kama wanavyodhani wahusika (au familia zao zingelijibu)
- Onesha maelekezo yafuatayo katika PawaPointi na elezea kwa waliojitolea kwamba watahitaji kupiga:

- **hatua mbili mbele ikiwa kuna uwezekano mkubwa wa tukio hilo kutokea/ uzowefu huo ni chanya;**
- **hatua moja mbele ikiwa tukio hilo linaweza kutokea/ uzowefu huo ni chanya;**
- **hatua moja nyuma ikiwa hakuna uwezekano wa tukio hilo kutokea/ uzowefu huo si chanya;**
- **hatua mbili nyuma ikiwa hakuna uwezekano  wa tukio hilo kutokea na uzowefu huo ni hasi.**

· Pia, majibu yao yawe kwa mujibu wa kile wanachokifikiria kwa sasa kuwa ni sahihi kulingana na hali pamoja na utamaduni wao– sio kile kinachopaswa kuwa.  Baada ya kila hatua na majibu ya waliojitolea, toa muda kwa washiriki wengine kutoa maoni yao. Kama washiriki hawakubaliani katika maoni yao, washiriki waamue kwa maafikiano na mshiriki aliyejitolea anaweza kuombwa kubadilisha msimamo wake.

· Andaa mazingira ya hadithi. ‘ Siku moja hapa Zanzibar baada ya subira ya kiasi miezi tisa muhusika wako anazaliwa. Jee wanafamilia walijisikiaje walipokuona wewe ni nani? Piga hatua

· Angalia kile ambacho kinaweza kutokea:

- familia ina furaha sana (mtoto wa kiume asiye na ulemavu amezaliwa), hatua mbili mbele;
- imefurahi ( mtoto wa kiume mwenye ulemavu/ mtoto wa kike asiye na ulemavu), hatua moja mbele;
- haina furaha (mtoto wa kiume mwenye ulemavu) hatua moja nyuma;
- haina furaha kabisa ( mtoto wa kike mwenye ulemavu), hatua mbili nyuma.

· ‘Sasa umekuwa, na ni wakati wa kuanza kufikiria kuhusu skuli. Kuna uwezekano gani wa wewe kuhudhuria skuli. Piga hatua’

· ‘Ungependa sasa kuendelea na elimu yako katika skuli ya sekondari. Kuna uwezekano gani wa wewe kuweza kundelea? Piga hatua’

· ‘Ungependa kundelea na elimu ya juu-chuo au chuo kikuu. Kuna uwezekano gani wa wewe kuweza kundelea? Piga hatua’

· ‘ Sasa una miaka 20. Ungependa kuwa katika ndoa. Kuna uwezekano gani wa wewe kuweza kufanya hivyo? Piga hatua’

- Ungependa kujishughulisha na kazi na unataka kujipatia kipato kwa ajili ya familia yako. Unajaribu kutafuta kazi. Je kuna wepesi kiasi gani kwako kupata hiyo kazi?
- 'Baada ya miaka kadhaa. Kila mmoja katika rika lako ana watoto. Kwa kiasi gani na wewe unaweza kulifikia hili? Angalia iwapo mtoto wa kike mwenye ukoma anapiga hatua mbili nyuma au anaelekezwa kufanya hivyo na washirki katika kikundi chake. Kwa nini ikatokea hivyo? Wanaweza kusema kuwa ni kwa sababu wanawake wengi wenye ulemavu kimaumbile hawawezi kupata watoto- imani potofu. Hatua mbili nyuma zinaweza kuwa ni jawabu sahihi kwa sababu tofauti –wanawake wenye uleamavu mara nyingi hawana watoto kwa sababu jamii inafikiri kuwa hawawezi kupata au hawapaswi kuwa na watoto.
- ' Sasa umri wako uko katika miaka 40. Una uzowefu wa kutosha katika maisha. Unataka kuisaidia jamii yako kwa kujishughulisha katika siasa za ndani. Ni kwa kiasi gani unaweza kufikia lengo hili?'
- Uliza washiriki:
  - Nani yuko katika nafasi nzuri zaidi sasa? Nani yuko katika nafasi mbaya?
  - Mliojitolea, jukumu hili limekufanya ujisikie vipi?
  - Je kuna jambo lolote lililomshangaza mshiriki yoyote?
  - Tunajifunza nini katika shughuli hii? (Karibisha majibu kutoka kwa washiriki mbalimbali.



*Washiriki kutoka Zanzibar wakicheza 'mchezo wa maisha'*

[Maelezo ya picha: watu sita (wanawake watano mwanamume mmoja anaetumia magongo ya kutembelea) wamesimama mbele huku wameshika karatasi nyeupe, nyuma yao kuna mwanamume alievaa kanzu nyeupe na miwani. Mbele yao kuna baadhi ya viti, mtu mmoja alievaa kanzu nyeupe amekaa katika mojawapo wa viti.]

- Fafanua nukta ifuatayo:

**Hali tofauti za kimaisha (kama vile pahali tulipozaliwa, familia tunayozaliwa, ikiwa ni mtoto wa kike au wa kiume au mwenye ulemavu), yote haya yako nje ya uwezo wetu, yana athari kubwa katika uwezo wetu wa kuepuka umasikini na kutengwa katika jamii.**

- Onesha uhusiano na Haki za Binaadamu–kila mmoja ana haki ya vitu vyote hivi – elimu, kuoa/kuolewa, lakini kuna sababu nyingi zinazopelekea haki hizo kutokupatikana
- Onesha slaidi ya 11 ya PawaPointi ya Kipindi cha 3 ‘Ubaguzi’

**PawaPointi** **PawaPointi Kipindi cha 3 ‘Haki za Binaadamu’**

- Waulize washiriki ni haki gani ya binaadamu wanafikiri inawakilishwa katika picha. Ikiwa hawaelewi, wape majibu. Haki za binaadamu zifuatazo zinaoneshwa.

**Baadhi ya mifano ya haki za binaadamu unazoweza kuanza nazo kwa washiriki**

1. Haki ya elimu
2. Haki ya kufanya kazi
3. Haki ya uhuru wa kujieleza
4. Haki ya ushiriki wa kisiasa
5. Haki ya uhuru wa kutembea
6. Haki ya kupumzika na starehe
7. Haki ya ulinzi wa kisheria

- Waulize washiriki, ‘Mnafikiri haki za binaadamu ni nini?’. Uliza iwapo kuna yeyote anayeweza kutoa ufafanuzi wa haki za binaadamu.
- Fikiria kuhusu maisha yako mwenyewe. Ni zipi kati ya haki zako za binaadamu zinaheshimiwa? Ni zipi unafikiri haziheshimiwi?
- Onesha slaidi ya 12 na 13 ya PawaPointi ya Kipindi cha 3 ‘Ubaguzi’.

**PowerPoint** **PawaPointi Kipindi cha 3 ‘Ubaguzi’**

- Wasilisha taarifa ifuatayo kwa washiriki:
  - Haki za binaadamu ni dhamana za kisheria zinazotumika kote ulimwenguni. Zinamlinda mtu mmoja mmoja na vikundi dhidi ya hatua (au wakati mwengine kutokuchukua hatua) ambayo inaingilia uhuru, haki, stahili na utu wao.
  - Kila mmoja ni **mwenye haki** –hii ina maana kwamba haki za binaadamu zinamuhusu kila binaadamu.
  - Sisi pia ni **watoa haki**. Hii ina maana kwamba sote tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba haki za binaadamu zinaheshimiwa, na hazivunjwi. Serikali zina wajibu mkubwa katika kuheshimu haki za binaadamu, kama ilivyo kwetu sisi kama wazazi na wanajamii. Kwa mfano, ukiwa kama mzazi, mwalimu au mwanajamii tuna wajibu wa kutoa haki ya elimu kwa kila mtoto.
- Karibisha maoni na mjadala kutoka kwa washiriki.

# Kipindi cha 4: Mfumo wa elimu ni nini?

**Ujumbe muhimu**

Mfumo wa elimu katika nchi nyingi ni wenye mambo mengi. Unajumuisha vipengele vingi vilivyoungana na vinavyohitaji kufanyakazi pamoja. Mfumo wa elimu pia unahitaji kuungana na sekta nyengine– hauwezi kufanyakazi kwa ufanisi bila ya mashirikiano na sekta nyengine.

## Maelezo kwa mwezeshaji

Takriban nchi zote zina mfumo wa elimu ambao umekusanya vipengele vingi kama vile:

- Sheria na sera zinazohusiana na haki na utoaji wa elimu;
- Mahakama na vyombo vyengine vya kulinda haki hizi
- Idara za serikali, timu au watu binafsi wanaohusika na vipengele mbalimbali vya elimu (mf.bajeti/fedha,mitaala, mitihani, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, maendeleo ya walimu na uajiri, miundombinu);
- Walimu na wahudumu;
- Viongozi wa skuli na wilaya, watawala, kamati;
- Vifaa vya elimu (mf.skuli, vituo vya walimu, vyuo, vyuo vikuu);
- Wanafunzi, wazazi,familia na wanajamii;
- Vipengele vyengine kama vile afya, usafiri, chakula/ teknolojia ya upishi.

Sehemu zote za mfumo huo zimeungana kwa kiasi fulani. Vitendo au mabadiliko ambayo yanatokea katika sehemu moja ya mfumo wa elimu inaweza kuathiri yanayotokea sehemu nyengine katika mfumo huo.

Majaribio ya kufanya mabadiliko katika sehemu moja ya mfumo unaweza usifnikiwe ikiwa mabadiliko kama hayo hayatokei katika sehemu nyengine ya mfumo (kwa mfano, jaribio la kuboresha zoezi la kufundisha na kujifunza katika skuli linaweza lisifanikiwe iki mitaala na mfumo wa mitihani au taratibu za kufanya tathmini hazibadiliki kulingana na zoezi jipya).hivyo, ili elimu iwe jumuishi tunahitaji vipengele vyote vya elimu vielekezwe njia moja.

Pia, mifumo ya elimu haiwezi kufanya kazi bila ya mashirikiano na sehemu nyengine za serikali na jamii. Kwa mfano, kuna haja ya kuwa na mashirikiano

na sekta za ustawi wa jamii, afya na sheria; sekta zinazoshughulikia ajira, biashara na uchumi; sekta zenye dhamana ya masuala ya michezo, utamaduni, mawasiliano na Habari; pamoja na sekta zinazoshughulikia uhamiaji na wakimbizi.

**Katika kipindi hiki washiriki :**

ü watafikiria vipengele mbalimbali vinavyounda mfumo wa elimu


ü watafikiria uratibu wa kisekta/ mashirikiano ambayo ni muhimu kwa elimu mjumuisho.

## Shughuli 4.1: Ramani ya mfumo wa elimu na muunganisho

1 Dakika 60

### Maelekezo

- Hakikisha unaweka tayari vipengele vyako vya mfumo wa elimu kutoka katika **Kielelezo 4.1a**
- Kwanza andika maneno 'Mfumo wa elimu katikati ya karatasi ya flipchati. Chora mistari kutokea katikati (kama vile unavyoanza kuchora mchoro wa ramani ya akili)– angalia pia mchoro ufuatao.




[Maelezo ya picha: Maneno 'Mfumo wa elimu' yaliyopo katikati yakigawika katika mistari kumi kutokea maneno hayo yaliyo katikati]

- Watake washiriki wataje vipengele vyote ambavyo vinaunda mfumo wa elimu. Unaweza kufanya shughuli hii katika vikundi vidogo vidogo, kwa jozi au kwa washiriki wote kwa pamoja.
- Wakati unapochukua majibu kutoka kwa washiriki bandika picha inayofaa kutoka **Kielelezo 4.1a** katika mchoro. Ikiwa washiriki watataja kipengele ambacho huna picha yake andika au chora kipengele hicho katika mchoro (ongeza visanduku katika mchoro kadiri itakavyohitajika).

**Kielelezo 4.1a** **Picha za vipengele mbalimbali vya mfumo wa elimu**

- Washajiishe washiriki kuvipanga pamoja vipengele vinavyohusiana au chora mistari inayoonesha muunganiko baina ya sehemu mbalimbali za mfumo wa elimu.
- Ikiwa itasaidia, linganisha mfumo wa elimu na mfumo wa mwili wa binaadamu ili kusaidia ufahamu Zaidi. Kwa mfano, viungo vyote vya mwili vinahitaji kufanya kazi kwa pamoja ili mwili uwe vizuri.
- Ongeza vipengele vyovyote muhimu katika mfumo walivyovisahau. Angalia mfano katika **Kielelezo 4.1b: Vipengele vya mfumo wa elimu.**
- Ikiwa una muda, waambie wachore mchoro mwengine unaoonesha secta nyengine zote ambazo mfumo wa elimu unahitaji kushirikiana nazo na sababu zake. Watake washiriki watoe mifano.
- Ongeza sekta nyengine, mbali na mfumo wa elimu, ambazo ni muhimu lakini wameziacha. Angalia mfano katika **Kielelezo 4.1c: Kushirikiana na sekta nyengine.**

# Kipindi cha 5: Elimu mjumuisho ni nini?

**Ujumbe muhimu**

Sote tunaweza kuwa na uzowefu na mawazo mbalimbali kuhusu elimu mjumuisho, lakini katika mtazamo halisi wa elimu mjumuisho, mwanafunzi kamwe sio tatizo; daima mfumo wa elimu ndio tatizo

## Maelezo  kwa mwezeshaji

Kila mshiriki atakuwa na mawazo tofauti kidogo kuhusu elimu mjumuisho, kutegmeana na kwa kiasi gani ameshasoma au kusikia, na pia inategemea taaluma au utaalamu wake. Shughuli ya kwanza katika kipindi hiki imesarifiwa kuwasadia washiriki waweze kutafuta zaidi kuhusu  mawazo ya kila mmoja wao na ili waweze kupata ya pamoja ya maana ya elimu mjumuisho.

Kipindi kitaendelea kutoa njia mbili tofauti sana ambazo tutazitumia kuona kutengwa kwa wanafunzi katika elimu kupitia  michoro ya ‘ mwanafunzi kama tatizo’ dhidi ya ‘mfumo wa elimu kama ni tatizo’. Kipindi hiki pia kitachunguza mifano zaidi ya elimu maalum, elimu mchanganyiko na elimu mjumuisho kupitia visa mafunzo na kitafafanua dhana potofu kuhusu tofauti ya elimu mjumuisho na elimu mchanganyiko.

**Katika kipindi hiki washiriki:**

ü Watabadilishana mawazo mbalimbali kuhusu elimu mjumuisho

ü Watajifunza kwamba ni mfumo wa elimu ndio unahitaji kubadilika, sio mwanafunzi

ü Watachunguza tofauti baina ya elimu maalum, ubaguzi, mchanganyiko na elimu mjumuisho kupitia visa mafunzo

## Shughuli 5.1: Mchoro: “Elimu mjumuisho inamaanisha nini kwangu”

1 Dakika 45

### Maelekezo

- Watake washiriki kila mmoja peke yake, bila ya mjadala, wachore mchoro wa kuonesha elimu mjumuisho ina maana gani kwao. Hii inaweza kuwa picha au mlolongo wa picha au mchoro.
- Watakapomaliza, kutegemea na muda uliopo unaweza kufanya moja kati ya yafuatayo:
  a) Mtake kila mshiriki ainue juu picha yake (mmoja baada ya mwengine) na aelezee kwa vipi picha yake inaleta tafsiri ya elimu mjumuisho.
  b) Wakiwa katika vikundi vidogo, watake washiriki waoneshane huku wakijadili michoro yao na wenzao kisha wachague mchoro ulio bora zaidi, sio lazima iliochorwa vizuri. Mchoro ulio bora zaidi kutoka kila kikundi utaoneshwa kisha ujadiliwe kwa pamoja na washiriki wote.
- Tumia karatasi ya flipchati kuandika **ujumbe muhimu unaohusu elimu mjumuisho** kama ulivyoainishwa na washiriki katika kipindi cha majadiliano. Baadae bandika michoro ukutani kwa ajili ya kutizamwa na kujadiliwa wakati wa mapumziko.
- Fanya majumuisho kwa kueleza kwamba, mchoro huu unatusaidia jinsi sote tunavyoweza kutafautiana katika kufafanua dhana ya elimu mjumuisho. Wakati tunapoifanyia kazi elimu mjumuisho, tutahitaji kuzifahamu tafauti hizo ili kuepuka kutokufahamiana na mkanganyiko usio wa lazima.



Mifano ya michoro iliyochorwa na washiriki

[Maelezo ya picha: Picha inayoonesha wanawake wawili wakionekana kubandika picha walizochora ukutani.]

## Shughuli 5.2: Tatizo liko wapi?

1 Dakika 60

**Ujumbe muhimu**

Mfumo wa elimu ndio tatizo kwa sababu hauna mnyumbuliko na ubunifu unaozingatia mahitaji ya wanafunzi mbalimbali. Mfumo ndio unahitaji kubadilika, sio mwanafunzi.

### Maelezo kwa mwezeshaji

Michoro miwili ifuatayo  inatoa njia mbili tofauti za kuangalia ubaguzi wa wanafunzi katika elimu.

Picha katika kurasa zifuatazo zinatoa njia mbalimbali za kuangalia kutengwa kwa wanafunzi katika elimu.

Mchoro wa kwanza unaonesha jinsi mfumo wa elimu ya jadi unavyowazingatia wanafunzi walio tofauti kwa kiasi fulani. Viduara vya mazungumzo vinanonesha namna ambavyo walimu katika skuli ambazo **si** jumuishi

zinavyoweza kuwapa majina wanafunzi ambao hawawezi kujifunza vizuri au hawapati mafaninkio, kwa mfano mwanafunzi mwenye mahitaji maalum ya kielimu au ulemavu. Katika mtazamo wa kijadi mwanafunzi anaonekana kuwa ni tatizo. Hii hupelekea skuli na walimu kujaribu kufikiria masuluhisho kwa kuleta mabadiliko kwa mwanafunzi, kujaribu 'kumtibu', au kwa kumfanya kwa namna fulani aweze kuendana na mfumo uliopo.


Mchoro wa pili unaonesha mtazamo mbadala. Hapa mwanafunzi sio tatizo. Mfumo wa elimu ndio tatizo kwa sababu hauko rafiki na hauna ubunifu wa kutosha kukidhi matakwa ya wanafunzi mbalimbali. **Mfumo ndio unahitaji marekebisho na sio mwanafunzi.**

## Maelekezo

- Onesha slaidi 1-picha inayoonesha mtazamo wa ' mwanafunzi kama tatizo' katika PawaPointi ya Kipindi cha 5 ' Elimu mjumuisho ni nini?

**PawaPointi** **PawaPointi ya Kipindi cha 5 ' Elimu mjumuisho ni nini?**

- Waulize washiriki, 'mnaona nini na mnajisikiaje mnapoangalia picha hii? Hakikisha pia unawaambia washiriki jinsi picha inayooneka ikiwa kutakuwa na mshiriki ambaye haoni vizuri. Unaweza kutumia maelezo ya picha: [Mtoto wa kike anakaa katika sakafu akiweka kichwa chake juu ya mikono yake na huwezi kuona uso wake. Mikono minne ikinyooshwa kumwelekea yeye kutokea pembe nne za picha. Kuna viduara vine vya mazungumzo katikati ya mikono. Viduara vya mazungumzo vinasema '' anahitaji vifaa maalum'', ''hafundishiki'', anajifunza ''polepole mno'', na '' hawezi kujifunza''.]
- Elezea namna mwanafunzi anavyoonekana kama ni tatizo katika mtazamo wa kijadi. Tumia maelezo ya mwezeshaji yaliyo hapo juu na maneno katika picha kwa ajili ya kukusaidia kutoa maelezo. **Pia jaribu kutoa mifano mingine katika jamii yako.** Si lazima kuwasilisha mchoro wa ' mwanafunzi kama tatizo' uliopo hapa chini, lakini unaweza kutumia baadhi ya mifano iliyomo katika mchoro huo.




[Maelezo ya picha: 'Mwanafunzi kama ni tatizo' katikati kwenye kisanduku na mistari inayoungana na kisanduku cha katikati Pamoja na visanduku vyengine saba pembeni mwake. Visanduku vimeanza upande wa kulia kwenda kushoto, kuanzia juu ikiwa ni pamoja na 1. Hajibu, hawezi kusoma; 2. Ana mahitaji maalum; 3. Anahitaji vifaa maalum; 4. Hawezi kufika skuli; 5. Ni tofauti na wanafunzi wengine; 6. Anahitaji mazingira maalum; 7. Anahitaji waalimu maalum.]

- Elezea kwamba katika mtazamo halisi wa elimu mjumuisho, mwanafunzi kamwe si tatizo, bali tatizo hasa ni mfumo wa elimu.

- Andika **'Mfumo wa Elimu ni tatizo' katikati** ya karatasi ya flipchati. Watake washiriki kutoa **mfano mmoja au miwili** ya matatizo katika mfumo wa elimu. Wahamasishe kufikiria tena katika vipengele vya mfumo wa elimu walivyovijadili kabla.
- Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 4 au 5. Gawa seti ya picha 10 kutoka **Kielelezo 5.2** kwa kila kikundi. Watake washiriki kuangalia picha na kujadili ni nini wanafikiri 'tatizo' katika mfumo wa elimu.

**Kielelezo 5.2** **Picha za 'matatizo' katika mfumo wa elimu**

- Kama kuna mshiriki yeyote mwenye ulemavu wa uoni, ni vyema kuzifafanua picha kwa ajili yao. Washiriki wengine wanaweza kufanya hivi au kutoa maelezo ya kila picha katika **Kielelezo 5.2.**
- Baada ya dakika 10-15, onesha slaidi ya 2 ya PPT ' Mfumo wa elimu kama tatizo' pamoja na picha zilizopo pembeni yake.  Katika majadala wa washriki wote jadili kila picha kwa **zamu** na kiambie kila kikundi kitoe mrejesho wa mfano mmoja au miwili kutoka katika mijadala yao ya kikundi. Picha zimejumuishwa kwenye mchoro kwa mpangilio sawa na picha katika **Kielelezo 5.2** zikisogea kwa mwendo wa saa( kulia kwenda kushoto) kutoka juu katikati, ikiwa utahitaji kutoa ufafanuzi. Washiriki watakuwa na picha mbili za ziada katika seti zao ambazo hazijaoneshwa kwenye mchoro kwenye slaidi 2. Hata hivyo, picha hizi zimejumuishwa katika 'maelezo ya mwezeshaji hapa chini.

**PawaPointi** **PawaPointi ya Kipindi cha 5 ' Elimu Mjumuisho ni nini?**

- Tumia maelezo ya mwezeshaji hapa chini ili kuongoza mjadala huu wa jumla. Picha hizo zinarejelewa kuwa za kutazama zile zilizo katikati ya juu ya mchoro na kusogea kimwendo wa saa (kama zilivyojumuishwa kwenye **Kielelezo 5.2**). Ni vizuri pia kama washiriki wamekuja na tafsiri tofauti za picha hizo na zile zilizoelezwa hapa chini.

## Maelezo ya mwezeshaji: kutoa mrejesho kuhusu mchoro wa ‘mfumo wa elimu ni tatizo’ pamoja na picha

**Picha ya 1: Mtoto wa kiume aliyevaa sare ya skuli , akiwa amechukua mkoba akipanda ngazi.** Mfano huu unaonesha jinsi baadhi ya watoto wanavyoweza kuendelea na kuingia katika ngazi mbalimbali za mfumo wa elimu huku wengine wakiachwa nyuma. Watoto wengine wenye ulemavu na watoto wa kike wanapofikia umri wa utu uzima) wanaachwa nyuma kwa wingi na mara nyingi huacha skuli.

**Picha ya 2: Watoto saba, wakiwa wamesimama katika foleni nje wakisubiri kwenda chooni.** Mfano huu unaonesha vipi ukosefu wa nyenzo katika skuli (ikiwemo vyoo) unaweza kuwaathiri Watoto. Pia, baadhi ya Watoto huathirika zaidi. Kwa mfano, Watoto wa kike mara nyingi hawahudhurii skuli wakati wa hedhi ikiwa hakuna vyoo vilivyo safi na salama ambapo wanaweza kubadilisha (taulo za kike) na vyoo ni nadra kuweza kufikiwa na watu wanotumia vitimwendo.

**Picha ya 3: Mtoto wa kiume amekaa katika kitimwendo akiwa hawezi kuingia darasani kwa sababu ya ngazi zilizopo nje ya mlango.** Mfano huu unaonesha jinsi jengo la skuli lilivyojengwa limesababisha mazingira yasiyofikika kwa watu wote.

**Picha ya 4: Mwalimu anafundisha hakuwaelekea wanafunzi (amewapa mgongo).** Mfano huu unaonesha kiwango duni cha ufundishaji ambacho hupelekea mahitaji ya wanafunzi kutofikiwa.

**Picha ya 5: Madaftari matatu yaliyopangwa , mstari, penseli, kalamu, raba, pamoja na mstari uliopita katikati.** Hii inaonesha upungufu wa vifaa na visaidizi katika maskuli.

**Picha ya 6: Mwalimu/Mwalimu mkuu akiwa nje ya skuli hamruhusu mwanafunzi wa kike kuingia kwa sababu hakuvaa sare ya skuli.** Mfano huu unaonesha jinsi sera zisizo nyumbulifu ( kwa mfano, watoto wote kulazimishwa kuvaa sare) zinavyoweza kuwaacha nyuma baadhi ya Watoto ikiwa familia zao haziwezi kununua sare.


**Picha ya 7: Darasa lenye wanafunzi wengi.** Hii inaonesha kwamba hakuna walimu wa kutosha kukidhi idadi ya wanafunzi na kupelekea madarasa kufurika wanafunzi na hivyo kutoruhusu matumizi ya njia shirikishi na jumuishi za ufundishaji.

**Picha ya 8: Picha mbili zilizotenganishwa na mstari mwekundu:** jengo lililoandikwa 'SERA ZA ELIMU' na wazazi/walezi wa Watoto wenye ulemavu. Picha hii inaonesha namna wazazi na walezi wasivyojishirikisha katika elimu ya Watoto wao na mara nyingi hawana uwelewa wa sera za elimu mjumuisho zilizopo. Hii ni kwa sababu skuli hizitekelezi sera hizo na au hazitambulishwi vizuri.

**Picha ya 9: Baba akikataa kuangalia kazi ya skuli ya mtoto wake wakati mwanawe akijaribu kumuonesha kazi hiyo.** Picha hii inaonesha ni namna gani wakati mwengine wazazi hawathamini elimu ya Watoto wao na hivyo hawawaungi mkono au kuwashajihisha Watoto wao ipasavyo.

**Picha ya 10: Wanafunzi wakiwa darasani wakiangalia kitabu cha mwanafunzi chenye taswira potofu kuhusu majukumu ya wanaume na wanawake.** Picha hii inaonesha kwamba mitaala inaweza kuwa imepitwa na wakati au si jumuishi, hasa ikiwa haihoji kuhusu Imani potofu kuhusu wanawake na wanaume au watu wenye ulemavuau makundi mengine ya watu.

- Ikiwa itasaidia, onesha mchoro wa pili wa 'Mfumo wa elimu kama tatizo' katika slaidi ya 3 (na hapa chini). Waambie washiriki kwamba mchoro huu unaonesha baadhi ya mambo yale yale ambayo tayari yameoneshwa kwa picha lakini pia baadhi ya mambo mengine ya ziada. Waulize **' ni matatizo gani ya ziada yaliyo katika mfumo wa elimu, ambayo yamenoneshwa katika mchoro huu, lakini hatujayataja hapa?'**
- Sisitiza kwamba katika mtazamo halisi wa elimu mjumuisho, mwanafunzi si tatizo; daima mfumo wa elimu ndio tatizo. Shughuli hii inakusudiwa kuwasaidia washiriki kutafakari kuhusu mawazo yaliyopo ambapo mwanafunzi anaonekana kuwa ni tatizo, lakini shughuli hii **isioneshe** kwamba mtazamo wa ' mwanafunzi ni tatizo' ni mtazamo sahihi au unaokubalika.




[**Maelezo ya picha:** Picha hiyo hapo juu inaonesha picha yenye mchoro ulioandikwa ‘ Mfumo wa elimu ni tatizo’ katikati katika kisanduku na mistari iliyoungana na kisanduku kilicho katikati pamoja na visanduku vyengine saba vikiwa katika mpangilio wa mwendo wa saa- kutoka kulia kwenda kushoto kuanzia juu ikiwa ni pamoja na 1. Mitazamo ya walimu inazuia mafanikio ya mwanafunzi, 2. Mbinu zisizobadilika, mitaala isiyozingatia mahitaji ya wanafunzi wote, 3. Mazingira yasiyofikika, 4. Wanafunzi wengi wameacha skuli, wanafunzi wengi wanarudia madarasa, inaonesha kwamba mfumo wa elimu unahitaji kuimarishwa, 5. Walimu na skuli hazisaidiwi ipasavyo na serikali na hivyo hawawezi kufikia mahitaji ya wanafunzi, 6. Wazazi/ walezi/ hawashirikishwi, 7. Ukosefu wa vifaa vya kufundishia, 8. Mafunzo duni ya walimu ina maana mahitaji ya wanafunzi hayazingatiwi ]....

## Shughuli 5.3: Je, hii ni elimu mjumuisho? Visa mafunzo

1 Dakika 75

### Maelezo ya mwezeshaji

- Elimu mjumuisho mara nyingi hudhaniwa kuwa na maana sawa na elimu mchanganyiko lakini hazifanani.
- Elimu mjumuisho inashughulikia zaidi ya kuwapigania watoto waliotengwa kufika skuli. Ni lazima pia waweze kushiriki na kupata mafanikio.
- Ili kila mtoto aweze kushiriki na kupata mafanikio, tunahitaji elimu bora, njia za kufundishia na kujifunzia zinazomzingatia mwanafunzi.

### Maelekezo

- Andaa mchezo wa kuwafanya washiriki kujigawa katika vikundi vipya
- Waambie washiriki kuwa tutachunguza tofauti baina ya elimu mjumuisho, mchanganyiko, ubaguzi na kutenga.
- Elezea kwamba 'elimu mjumuisho' ni neno linalotumika kuelezea njia mbalimbali na tofauti katika elimu –baadhi yake sio jumuishi. Sote tunapaswa kufikiri iwapo yale **tunayoyatenda** yanaendana na yale **tunayoyasema**. Hii ina maana kujikumbusha kuhusu tofauti baina elimu maalum, elimu mchanganyiko na mjumuisho.
- Wape washiriki katika vikundi vyao kitini kifuatacho na waambie tutaangalia mifano mingine tofauti

**Kitini 5.3** **Visa mafunzo 'Je, hii ni elimu mjumuisho?'**

- Watake washiriki wasome mfano wa kisa mafunzo katika kitini. Mshiriki mmoja anaweza kusoma kwa sauti kwa wengine ikiwa hii itasaidia. Baadae wajadili maswali (PPT Kipindi cha 5 slaidi ya 4)
  - **Je, unadhani kila mfano unaonesha elimu mjumuisho, au elimu mchanganyiko, au ubaguzi, au kutengwa? Kwa nini unafikiri hivyo?**
  - **Unafahamu nini kuhusu maneno haya? Unakubaliana na maana ya maneno haya?**
- Onesha PawaPointi ya kipindi cha 5 ' Elimu Mjumuisho ni nini? slaidi ya 4 tu.


PawaPointi

**PawaPointi ya Kipindi cha 5: Elimu Mjumuisho ni nini?**


- Washiriki watataka uwaambie 'jawabu'lakini washajiishe kuchukua muda kujadiliana na kuwaeleza wengine kuhusu mjadala wao
- Baada ya dakika 20, Sitisha  kazi za vikundi. Kisha onesha na elezea mchoro uliopo katika slaidi za 5-8 moja baada ya moja. Ruhusu muda wa mjadala na maswali.

## Elimu maalum au ubaguzi

Kuna mfumo wa elimu kwa wanafunzi 'wa kawaida' (vipande vya duara); na mfumo tofauti kwa wanafunzi wenye 'mahitaji maalum'(vipande vya mraba).



Skuli ya 'Kawaida'




Skuli maalum

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo mviringo  na vipande vidogo vidogo vya mviringo vikipita katika vishimo hivyo. Hii inawakilisha skuli ya kawaida. Kipande chengine cha ubao kina vishimo vya mraba na vipande vidogo vidogo vya mraba vikipita katika vishimo hivyo. Hii inawakilisha skuli maalum. Vipande vidogo vidogo vya mraba na mviringo vinawakilisha wanafunzi]

## Mchanganyiko

Hapa watu wanajaribu kubadilisha wanafunzi ili waendane na mfumo unaoitwa wa 'kawaida'(kuvirekebisha vipande vidogo vya mraba viweze kupita katika vishimo vya mviringo). Mfumo wa elimu na utaratibu wa ufundishaji na ujifunzaji haubadiliki. Kwa hivyo, mwanafunzi ni lazima abadilike au ashindwe kufaulu.




Skuli mchanganyiko

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo mviringo na vipande vidogo vidogo vya mviringo vikipita katika vishimo hivyo. Kipande kimoja kinakosekana. Pembeni yake kuna kipande kidogo cha mraba ambacho kinawakilisha mwanafunzi wa skuli maalum. Kipande hiki kinarekebishwa ili kiwe na umbo la mviringo na kiweze kuingia katika vishimo vya mviringo. Mchoro huu unawakilisha skuli mchanganyiko.]

## Elimu Mjumuisho

Hapa, wanafunzi wote ni tofauti na wote wanaweza kusoma hapa kwa kadiri ya uwezo wao. Mfumo wa elimu umebadilishwa kuweza kushughulikia wanafunzi wote. Mfumo huu unatatua vikwazo vyake vya kujifunza na kushiriki, ikiwa ni kwa sababu ya mitazamo, mazingira duni, mazoea na sera zisizofaa, au ukosefu wa nyenzo.



Skuli mjumuisho

[Maelezo ya picha: Mchoro huu unaonesha kipande cha ubao chenye vishimo vya maumbo mbalimbali na vipande vidogo vidogo mbalimbali vikipita ndani ya vishimo hivyo.]

- Waambie washiriki warejee katika vikundi vyao na kuuliza “Sasa kwa kuwa umeona baadhi ya ufafanuzi, je, umebadilisha maoni yako kuhusu kila

hadithi inavyowakilisha ujumuishi, mchanganyiko, na kutengwa? Ikiwa ndivyo, kivipi? Kwa ufupi jadilini tena katika vikundi vyenu".

- Baada ya dakika 10-15 chukua mrejesho kutoka kwa washiriki wote, ama kwa kusoma kila kisa kwa zamu na kukaribisha majadiliano au kwa kuvitaka kila kikundi kuelezea majibu yao kwa zamu kwa kila kisa mafunzo kimoja na baadae kukaribisha majibu kutoka vikundi vyengine.
- Kwa baadhi ya visa mafunzo, inawezekana kusiwe na jibu moja sahihi. Iwapo washiriki watatoa jibu lenye mantiki na lililojengewa hoja vizuri, ambalo haliwiani kabisa na majibu yaliyo hapa chini, lakini jibu hilo sio kosa moja kwa moja, basi mwezeshaji asiwaambie kuwa wamekosea. Badala yake, mwezeshaji awasilishe jibu lake mwenyewe na kuwataka washiriki kujadili kama wanakubaliana na jibu hilo (na kwanini/ kwa nini hawakubaliani nalo)
- Sanduku lifuatalo linatoa muongozo wa majibu kwa mwezeshaji.

**Hadithi ya 1– Kutengwa** –lakini sio lazima kwa kukusudia. Mwalimu mkuu alikuwa akijaribu kutatua tatizo lililokuwa liksababisha watoto wa kike kutengwa skuli, lakini kwa bahati mbaya suluhisho hilo pia lilisababisha kutengwa.

**Hadithi ya 2–Elimu mchanganyiko–** mwalimu anawaruhusu watoto ambao hawajifunzi vizuri wabakie darasani mwake, lakini hafanyi mabadiliko katika ufundishaji wake, kwa hivyo watoto hawa wanahudhuria skuli bila ya ushiriki au kujifunza. Hakuchukua jitihada zozote kuwa jumuishi zaidi (kwa mfano, kubadilisha ukaaji). Alivunjika moyo kwa kutokuwa na matokeo mazuri, badala ya kujaribu kufikiria suluhisho jengine tofauti.

**Hadithi ya 3– Kutengwa na kubaguliwa –** watoto wa kiume walirejeshwa nyumbani lakini waliishia mitaani. Suluhisho lilikuwa kuwabagua (wasome peke yao), lakini suluhisho hili halikufaa na wakaacha skuli, kwa hivyo wametengwa tena.

**Hadithi ya 4 – Elimu mjumuisho** – mwalimu anatumia usaidizi-rika kumsaidia Yusuf, anakubali kufanya tathmini aina mbalimbali, na kubuni mbinu mbalimbali za kumsaidia Yusuf na watoto wengine kwa kuwapa usaidizizi wa ziada inapohitajika.

**Hadithi ya 5 – Elimu mchanganyiko** – Halima anaruhusiwa kuwepo darasani lakini mwalimu hafanyi mabadiliko ya kumsaidia aweze kushiriki na kujifunza kikamilifu.

- Rejea katika hadithi ya 5. Zungumzia yafuatayo:

> ''Hadithi hii ni mfano wa mchanganyiko. Hii ni kwa sababu mwalimu wa Halima amemruhusu kuingia darasa la kawaida, lakini halima hashiriki kikamilifu au kujifunza. Mwalimu wake haangalii kujifunza kwake kwa uzito au kuzingatia mbinu zinazomlenga mwanafunzi ili kumshirikisha na kumuunga mkono Halima. Halima amekaa tu hafanyi chochote. Hashiriki na hafanikiwi chochote. [kielimu au kijamii]. Katika kufafanua maana yetu ya elimu mjumuisho tunaelewa kuwa elimu mjumuisho ni wakati wanafunzi wote **wapo, wanashiriki** na **wanafaulu**. Ikiwa wapo tu basi elimu mjumuisho ingawa mradi/skuli inaweza kuonekaana kuwa angalau inasonga mbele katika muonekano sahihi.''

- Onesha slaidi ya 9 – 11 ya Pawapointi ya Kipindi cha 5: 'Elimu mjumuisho ni nini?'

**PawaPointi** **Kipindi cha 5: Elimu Mjumuisho ni nini?**

Maelezo ya picha kwa slaidi ya 10 na 11 yanapatikana hapa chini:

**[Maelezo ya picha1:** Mbele watoto wawili, mmoja mwenye ualbino, wamekaa sakafuni wakicheka na kuna kuna karatasi kubwa baina yao kukiwa na maandishi na michoro katika karatasi hiyo. Nyuma yao kuna watoto wawili, mmoja wa kike na mwengine wa kiume anayetumia magongo, wanabandika ukutani bango lenye maandishi na michoro. Upande wa kulia watoto watatu wamekaa katika deski kila mmoja upande wake na mwalimu anatabasamu na ameegemea deski. Wote wako darasani ambako kuna na karatasi zenye maandishi na michoro zilizobandikwa katika kuta]

**[Maelezo ya picha ya 2:** Watoto watatu wanacheza katika uwanja wa kuchezea wa skuli. Jengo la skuli linaonekana nyuma. Mtoto mmoja wa kike aliyevaa hijab ameshikilia upande mmoja wa kamba ya kurukia na mtoto wa kiume aliye katika kitimwendo amekamata upande mwengine. Mtoto wa tatu anaruka kamba. Wote wanatabasamu.]

# Kipindi cha 6: Vikwazo vya ujumuishaji katika elimu

**Ujumbe muhimu**

Vikwazo vikubwa vya ujumuishaji wa kila mmoja katika elimu sikuzote si lazima view vya kimazingira–vinaweza kusababishwa na mitazamo hasi, au kutokana na sera za kibaguzi za serikali au skuli, au mazoea ya ufundishajo ambayo hayawezeshi ushiriki wa wanafunzi wote.

## Maelezo ya mwezeshaji

Tunafikiria kuhusu vikwazo vya ujumuishaji, mara nyingi huwa tunafikiria kuhusu vikwazo vya kimazingira kama vile ngazi na kukosekana kwa baraza mtelezo (rampu). Hata hivyo, vikwazo vikubwa vya ujumuishaji katika elimu inawezekana sio vya kimazingira tu–vinaweza kusababishwa na mitazamo hasi, au kutokana na sera za serikali au skuli ambazo zina ubaguzi, au kwa mazoea ya ufundishaji ambayo hayawezeshi wanafunzi wote kuweza kushiriki, au kutokana na ukosefu wa rasilimali watu na vifaa. Baadhi ya vikwazo vinahitaji pesa ili tuweze kuviondoa (kama vile kujenga baraza mtelezo au kuchapisha vitabu vinavyoweza kufikika). Hata hivyo, vikwazo vingi vinaweza kuondolewa bila ya kutumia pesa nyingi, lakini badala yake tunaweza kutumia fedha chache zilizopo kwa uangalifu katika kutafuta suluhisho lisilo na gharama kubwa.

Ili kuelewa kwa undani zaidi sababu zinazowafanya baadhi ya wanafunzi kutohudhuria au kujiunga na skuli, tunahitaji kuchambua vikwazo (vizuizi) vinavyowakabili. Kipindi hiki kitasaidia washiriki kuelewa kikwazo cha ujumuishaji ni nini, ni mambo gani yanaweza kuwa vikwazo na ni vipi vikwazo hivi vinawaathiri wanafunzi. Hii ni hatua muhimu ya kuchukua kabla ya kuanza kutafuta njia ya kuondokana na vikwazo hivi na hivyo kuwajumuisha wanfunzi wengi zaidi.

### Katika kipindi hiki washiriki:

- Watachunguza aina mbalimbali za vikwazo vya elimu mjumuisho na kujifunza jinsi ambavyo mitazamo hasi ni moja kati ya vikwazo vikuu.
- Watelewa kwamba watu mbalimbali(wanafunzi, wazazi, wanaweza kutofautiana katika kutafsiri vikwazo  vya elimu mjumuisho)

## Shughuli ya 6.1: Tunamaanisha nini tunaposema vikwazo vya ujumuishaji?

1 Dakika 45

**Maelekezo:**

- Elezea kwamba tunapoanzisha elimu ambayo ni jumuishi, yenye ubora na iliyo Rafiki kwa mwanafunzi, tunahitaji kuwa na mawazo ya kina juu ya changamoto (vikwazo) vilivyopo, ili tuweze kutafuta suluhisho sahihi linaloendana na muktadha.
- Elezea kwamba vikwazo si siku zote ni rahisi kuviona, vinajumuisha mambo mengi, na watu mbalimbali wanaweza kuvielewa na kutoa kipaumbele kwa vikwazo tofauti vya ujumuishaji hata katika mazingira yaliyo sawa sawa.
- Pia tumeshajadili, pia tunahitaji kufikiria kuhusu vikwazo hivi kupitia mkabala wa kijamii –i.e., fikiria kuhusu matatizo katika jamii na/au mfumo wa elimu ambao unawasababisha wanafunzi kutengwa.
- Watake washiriki kufikiri kuhusu aina za vikwazo vya elimu ambavyo wamevipitia. Wape muda kujadili haya katika vikundi vyao.
- Chukua mrejesho kutoka kwa washiriki na jaribu kuvigawa vikwazo hivi wanavyovitaja katka maeneo sita: **mazingira, mitazamo, sera, matendo, habari na nyenzo.**
- Watake washiriki waangalie nyuma katika picha 10 za 'tatizo' walizozijadili hapo kabla. Wape tena picha hizo ikiwa ulizikusanya hapo awali. Waambie vikundi waangalie picha na waziweke picha katika maeneo sita yaliyorodheshwa awali. Baadhi ya picha, huenda zikaonesha kikwazo zaidi ya aina moja. Wape dakika 10-15 kujadili.

**Kitini 6** picha za vikwazo

- Onesha PawaPointi ya Kipindi cha 6: 'Vikwazo vya Elimu Mjumuisho?' slaidi 1-6

**PawaPointi** Kipindi cha 6: Vikwazo vya Elimu mjumuisho?

- Elezea aina mbalimbali za **vikwazo ukigusia** mifano mbalimbali kama ilivyotolewa katika picha ( Katika slaidi za PPT) na kwa kuongeza mifano yako mwenyewe.

- **Vikwazo vya kimazingira.** Hivi ni pamoja na majengo ya skuli, mazingira ya nje na vyoo ambayo hazifikiki au haziko salama, mazingira chini ya kiwango au ya hatari.
- **Vikwazo vya kimtazamo.** Hivi vinajumuisha mitazamo hasi kwa utofauti na imani potofu kwa watu, matarajio madogo kwa baadhi ya wanafunzi ambapo hupotosha tathmini ya mwalimu kwa mahitaji na uwezo wa mwanafunzi; mwasiliano yasiyo sahihi; kutokuthamini uzowefu wa wanafunzi na wazazi/walezi/ ambao wanaweza kuuleta katika skuli ; na kushindwa kuwashrikisha wazazi/walezi na jamii kwa ujumla katika skuli na shughuli zake mbalimbali.
- **Vikwazo vya kisera.** Hivi ni pamoja na miundo ya kujifunza isiyobadilika; mitaala finyu isiyozingatia uzowefu wa wanafunzi au matayarisho yao ya kufanya kazi baada ya masomo; sera zisizofaa pamoja na sheria zisizozingatia mahitaji ya kielimu kwa wanafunzi wanaotoka katika familia zenye kipato cha chini. ( Mfano wa 1: sera ya skuli ya kulazimisha wanafunzi wote kuvaa sare na kuwaadhibu au kuwarejesha nyumbani wale ambao hawatavaa sare ya skuli. Mfano wa 2: Watoto wanaolazimishwa kurudia madarasa au kuacha skuli bila ya kupatiwa usaidizi unaostahiki katika mazingira jumuishi utakaowawezesha kuendelea na masomo yao vizuri.)
- **Vikwazo vya Kimazoea.** Hivi ni pamoja mafunzo duni au yasiyotosheleza ya walimu na viongozi wa elimu; ukosefu wa uwelewa kuhusu njia bora za ufundishaji; ukosefu wa uwelewa wa mikakati ya kuunga mkono mitaala na ujifunzaji wa lugha ya pili ambayo siyo lugha mama ya wanafunzi.
- **Vikwazo vya rasilimali.** Hivi ni pamoja na upungufu wa walimu; mrundikano wa wanafunzi madarasani; huduma hafifu na zisizotosheleza, ikiwemo huduma za msaada wa kilugha au kujifunza kwa walimu na wanafunzi.
- **Vikwazo vya taarifa:** Ukosefu wa taarifa kwa baadhi ya wazazi kwamba Watoto wao wanaweza kusajiliwa katika skuli iliyo karibu na makaazi yao, sera za elimu mjumuisho kutotekelezwa ipasavyo katika skuli na familia kuokuelewa kuhusu sera hiyo.
- Mwisho, sema yafuatayo:
  - Tunapofikiria kuhusu vikwazo vya ujumuishaji, aghlabu huwa tunafikiria vikwazo vya kimazingira, kama vile ngazi na ukosefu wa rampu.
  - Hata hivyo, kikwazo kikubwa cha ujumuishaji katika elimu si lazima iwe ni mazingira, – inaweza kusababishwa na mitazamo hasi, au sera za kibaguzi za serikali na skuli au mazowea ya ufundishaji yasiyozingatia mbinu za kuwashirikisha wanafunzi wote.

- Tunahitaji fedha kuondoa baadhi ya vikwazo (kama vile rampu katika majengo au kuchapisha vitabu vinavyoweza kusomwa na wote).
- Hata hivyo, kuna vikwazo vingi ambavyo vinaweza kuondolewa bila ya kutumia fedha nyingi, badala yake tunahitaji kutumia kwa uangalifu fedha tuliyonayo au kutafuta masuluhisho yasiyo na gharama kubwa.

## Shughuli ya 6.2 Kutumia picha kutafakari elimu mjumuisho

1 Dakika 60

Picha zinaweza kusaidia sana katika kuchangamsha washiriki katika kujadili masuala ya ujumuishaji, na kutafakari juu ya uzowefu na mawazo yao wenyewe. Hii inaitwa uhamasishaji kwa kutumia picha.

**Kielelezo 6.2** **Picha**

**Maelekezo:**

- Toa seti kamili ya picha kwa kila kikundi cha washiriki.
- Waambie washiriki wajadili iwapo wanadhani kuwa pich hizo zinaonesha elimu mjumuisho au la.
- Je, wanaweza kubaini angalau picha kikwazo kimoja cha ujumuishaji katika kila picha? Vikwazo hivyo ni vya kimazingira, sera, mitazamo, habari, mazowea au rasilimali au mchanganyiko wa vikwazo hivi.
- Watake washiriki pia kungalia mifano ya masuluhisho ya elimu mjumuisho katika picha. Kutokukubaliana ni sawa kwa sababu hakuna jawabu sahihi na isiyo sahihi.
- Ongoza utoaji wa mrejesho kuhusu picha kwa washiriki wote, kwa kutumia moja kati yan jia zifuatazo:
  a. Onesha picha moja moja na waalike washiriki kutoa majibu yao. Ikiwa kutakua na washiriki wasioona, utahitaji kuhakikisha maelezo yanatolewa kwao pia.
  b. Wakaribishe washiriki katika vikundi vyao wawasilishe majibu yao kuhusu picha mbalimbali na kisha waruhusu washiriki wengine kutoa maoni yao, kujadili au kutokukubaliana.

- Hitimisha kwa kuonesha baadhi ya makusdio ya wanafunzi wakati wa kupiga picha.
- Elezea jinsi shughuli hii inavyoonesha kwamba kila mmoja ana tafsiri mbalimbali za hali Fulani. Wanafunzi, wazazi/walezi etc. wote wanaweza kutafsiri hali hiyo hiyo katika njia tofauti na kupelekea mawazo mbalimbali kuhusu vikwazo na ufumbuzi wake. Kuwaruhusu wanafunzi kupiga picha za uzowefu wao wa kujumuishwa au wa kubaguliwa mara nyingi hupelekea kupata mahitimisho tofauti na yale watu wazima wanayofikiri kuwa ni 'sahihi ' kwa wanafunzi.

# Kipindi cha 7: Utetezi wa elimu mjumuisho

**Ujumbe muhimu**

- Utetezi unahusu kuchukua hatua za kuleta mabadiliko na sisi sote tunakuwa ni watetezi wakati tunapofanya jambo la kuleta mabadiliko, hata kama ni dogo.
- Mara nyingi utetezi huhusisha kuwasaidia watu kupaza sauti zao katika kuleta mabadiliko katika namna ambavyo watu hufikiri (mitazamo) na namna ambavyo mambo yanafanywa(mazowea).

## Maelezo ya mwezeshaji

- Mara nyingi utetezi hunekana ni  kitu ambacho watu walio katka nafasi za uongozi tu ndio wanaohusika nayo na kwamba utetezi unahitaji kiwango cha juu cha maarifa na ujuzi.
- Kipindi hiki kinahusu namna ya kuanza kujenga maarifa na uwelewa kuhusu utetezi has ani kitu gani n ani kwa vipi kila mmoja wetu ana nafasi ya kuwa mtetezi.
- Kitalenga katika kuwafanya washiriki watafakari maisha yao na jamii zao wenyewe na kuwataka wafikirie ni vipi walifanya utetezi kuleta mabadiliko, hata kama yalikuea ni madogo sana.
- Kipindi hiki pia kitatambulisha  ujuzi/stadi muhimu ambazo washiriki wanaweza kuzitumia ili kuwa na ufanisi katika utetezi. Hii itawasidia wao kupanga mipango yao ya utetezi wa masuala ya elimu mjumuisho katika jamii zao.
- Kipindi kitatumia hatua za CHUNGUZA, FIKIRI& CHUKUA HATUA za utafiti tatuzi  kuwatambulisha washiriki katika ujuzi/stadi za utetezi. Baadaye tutatumia hatua hizi katika kuimarisha uandaaji wa hatua za utetezi.

### Katika kipindi hiki washiriki:

ü watachunguza maana ya utetezi

ü watatafakari njinsi ambavyo wamekuwa wakifanya utetezi katika maisha yao

ü watajifunza baadhi ya ujuzi/stadi muhimu zambazo ni muhimu katika kufanikisha kazi ya utetezi

## Shughuli ya 7.1 Utetezi ni nini?

1 Dk 60

### Maelekezo

- Anza kipindi kwa kuhakikisha kuwa kila mshiriki ana kadi mbili za karatasi zenye rangi tofauti(mf. Manjano na wardi)
- Weka karatasi mbili za flipchati ukutani na juu ya moja wapo andika ‘‘ nilichotaka kubadilisha (suala) ’’  na katika karatasi nyengine andika ‘‘ nilichofanya katika kuleta mabadiliko(hatua)’’
- Tambulisha kipindi kwa washiriki kwa kufungua

**PawaPointi** **PPT Kipindi cha 7**

- Pitia slaidi 3 za PPT za mwanzo. Slaidi hizi zinatambulisha dhana ya utetezi kwa kuwasilisha ujumbe mwepesi wa kuelezea utetezi ni kitu gani.
- Baada ya kuzipitia slaidi hizi weka slaidi ya 4 (picha ya jingo la bunge na watu wakifanya utetezi)
- Waambie washiriki waangaliepicha (au maelezo yake) na wabdilishane mawazo kuhusu kinachoendelea katika picha mbili hizo. Maelezo ya picha yapo hapa chini:
- [Picha ya 1: kikundi cha watu kimekaa katika viti vilivyopangwa kama ngazi wakitazamana na msemaji ambaye haonekani katika picha. Katika kikundi hiki kuna mwanamke aliye katika kiti cha magurudumu akinakili maelezo, mwanamme mmoja mwenye ualbino mikono yake ameielekeza juu na mwanamke mwengine aliyevaa hijabu ambaye amesimama na amenyanyua mkono wake mmoja. Neno BUNGE limeandikwa kwa herufu kubwa hadi mwisho wa picha hiyo. Pichay a 2: Watu wawili waliosimama wanazungumza. Mwanamke aliye upande wa kulia anatumia mikono yake kufanya alama kwa mwanamme aliyeko upande wa pili aliyekunja mikono yake.  Mwanamke aliyeko katikati amevaa hijab akiwa anaangalia. Nyuma ya picha kunaonekana maduka na msikiti na mtoto wa kike alivaa kanzu yenye rangi ya zambarau akimwendesha mtoto wa kiume aliyekaa katika kiti chake cha magurudumu.]

- Eleza kwa washiriki kuwa sasa tutatafakari nyakati ambazo wao katika historia za maisha yao walifanya kati ya utetezi.
- Waambie kuwa hakuna majibu sahihi na yasiyokuwa sahihi katikazoezihili – washiriki wazingatie muda ambao walijaribu kuleta mabadiliko ya kitu fulani kwa sababu tulidhani kulikuwa na haja ya mabadiliko kukifanya kiwe bora zaidi.
- Watake washiriki wachukue **kadi za manjano** na kuandika **SUALA moja** lilitokea wakati uliopita ambapo waliona jambo fulani na wakahisi haja ya kutaka mabadiliko katika jamii yao na wakafanya kitu katika kuleta mabadiliko hayo.
- Waeleze washiriki kuwa jambo hilo linaweza kuwa ni kitu kidogo tu (mf. Kuona kuwa watoto wa jirani kutokuwa na chakula (kwa sababu mama yao kila siku alilazimika kuchelewa kurudi na hivyo watoto hawakuweza kupata chakula mpaka mama yao aliporudi) AU kitu kikubwa kama kuona kuwa kuna njia mbovu ambayo inazuia watu kuifikia skuli ya karibu wakati msimu wa mvua)
- Waambie washiriki kuwa ikiwa kuna mtu yeyote ambaye hawezi kuandika suala lake katika kadi kuwa utamsaidia, au aombe msaada kwa mshiriki mwengine.
- Baada ya kuliandika suala hilo waambie wachukue kadi ya rangi ya wardi na waandike **HATUA** ambayo alichukua katika kujaribu kuleta mabadiliko kwa waliyoyaona (mf. Alizungumza na jirani kumruhusu aweze kuingia ndani na kuwapashia moto chakula alichokiacha mama na akawpikia chakula cha ziada AU alitayarisha mkutano kuzungumza na Sheha kuomba msaada wake ili kuihimiza serikali kutengeneza njia iliyoharibika.
- Baada ya kila mshiriki kumaliza kadi zake zote mbili, watake wapeane taarifa na mshiriki aliye karibu naye kuhusu SUALA lake na HATUA aliyoichukua. Waulizane maswali ili kila mmoja aelewe vizuri.
- Kisha, mwombe kila mmoja abandike kadi zake katika karatasi mbili za flipchati–za manjano ziwekwe katika flipchati ya ‘masuala’ na za wardi katika ‘hatua’ (Slaidi ya 5 ina maswali haya)
- Waombe washiriki wasogee hadi zilipo kadi na soma baadhi ya mifano iliyotolewa. Ikiwa maandishi ni madogo sana au baadhi ya washriki hawawezi kusoma, soma mifano michache kwa washiriki wote.
- Waeleze washiriki kuwa jambo hilo linaweza kuwa ni kitu kidogo tu (mf. Kuona kuwa watoto wa jirani kutokuwa na chakula (kwa sababu mama yao

kila siku alilazimika kuchelewa kurudi na hivyo watoto hawakuweza kupata chakula mpaka mama yao aliporudi) AU kitu kikubwa kama kuona kuwa kuna njia mbovu ambayo inazuia watu kuifikia skuli ya karibu wakati msimu wa mvua)

- Waambie washiriki kuwa ikiwa kuna mtu yeyote ambaye hawezi kuandika suala lake katika kadi kuwa utamsaidia, au aombe msaada kwa mshiriki mwengine.
- Baada ya kuliandika suala hilo waambie wachukue kadi ya rangi ya wardi na waandike **HATUA** ambayo alichukua katika kujaribu kuleta mabadiliko kwa waliyoyaona (mf. Alizungumza na jirani kumruhusu aweze kuingia ndani na kuwapashia moto chakula alichokiacha mama na akawpikia chakula cha ziada AU alitayarisha mkutano kuzungumza na Sheha kuomba msaada wake ili kuihimiza serikali kutengeneza njia iliyoharibika.
- Baada ya kila mshiriki kumaliza kadi zake zote mbili, watake wapeane taarifa na mshiriki aliye karibu naye kuhusu SUALA lake na HATUA aliyoichukua. Waulizane maswali ili kila mmoja aelewe vizuri.
- Kisha, mwombe kila mmoja abandike kadi zake katika karatasi mbili za flipchati–za manjano ziwekwe katika flipchati ya 'masuala' na za wardi katika 'hatua' (Slaidi ya 5 ina maswali haya)
- Waombe washiriki wasogee hadi zilipo kadi na soma baadhi ya mifano iliyotolewa. Ikiwa maandishi ni madogo sana au baadhi ya washriki hawawezi kusoma, soma mifano michache kwa washiriki wote.
- Waulize washiriki wote kitu gani wamejifunza katika kufanya shughuli hii.

## Shughuli ya 7.2: Stadi muhimu za utetezi mzuri

### Shughuli ya 7.2 (i): Kutumia utafiti tatuzi kwa utetezi mzuri

1 Dakika 15

### Maelekezo

- Waoneshe washiriki slaidi ya 6 ya PPT. Slaidi hii inaonesha mzunguko wa utafiti tatuzi, ukihusisha hatua tatu za kuchunguza (kuangalia), kufikiri na kuchukua hatua.

**PawaPointi** **PPT Kipindi cha 7**

- Ioneshe slaidi hiyo na uwatake washiriki kila mmoja azungumze na aliye karibu naye ni kitu gani wanadhani kinatokea katika mchoro kwa kila moja kati ya michoro midogo. Wape kiasi dakika 5 kujadili mchoro huo.
- Baada ya dakika 5 watake watoe maoni yao kwa pamoja kuhusu kinachotokea katika kila mchoro mdogo (kila sehemu ya mzunguko). Andika yanayojitokeaza katika flipchati. Chukua kiasi dk 5 kwa ajili ya mrejesho.
- Waeleze washiriki kuwa sasa tutafanya shughuli ya kuchunguza na kutumia utafiti tatuzi.

## Shughuli ya 7.2(ii) KUCHUNGUZA vikwazo na msaada katika elimu mjumuisho

1 Dk 15

## Maelekezo

- Waeleze washiriki kwamba sasa tutaangalia video fupi kuhusu vikwazo ambavyo watoto wenye ulemavu wanaweza kukabiliana navyo wakati wa kwenda skuli asubuhi.
- Waambie wafikiri kuhusu maswali mawili ( Slaidi ya 7) wakati wanaanglaia video hiyo.
  - **Swali la 1**: Je, katika video hii aina zipi za vikwazo mbalimbali ambavyo watoto wanakabiliana navyo wakatii wa kwenda skuli?
  - **Swali la 2:** Kuna mifano gani katika video hii ambapo watu wengine au wanajamii walifanya kitu kusaidia watoto na kuondoa vikwazo walivyokuwa navyo?
- Sasa chezesha video ya EENET: 'Siku Jumuishi: Programu ya 2: Kufika skuli' kutoka katika flash diski (dk 8)

**Kitini 7.1** **Mafunzo ya EENET ya ualimu kuhusu ujumuishaji kwa kutumia vide: Kufika skuli**

- Baada ya kuangalia, kwa ufupi watake washiriki wote watoe majibu yao. Unaweza kuuliza maswali haya:
  - Je, waliweza kutambua matukio hayo? Je, katika jamii zao wanayo matukio kama yaliyomo katika video?

- Kitu gani kimewavutia sana katika video? Kwa nini?

## Shughuli ya 7.2 (iii) KUFIKIRI kuhusu vikwazo na msaada wa elimu mjumuisho

1 Saa 1 dk 45

### Maelekezo

- Watake washiriki wagawike katika vikundi vya watu 4-5 ( Kila kikundi kiwe na watu 4-5)
- Toa kwa kila kikundi karatasi za flipchati na kalamu za rangi mbalimbali.
- Elezea kwamba sasa tutatengeneza mchoro wa mlima. Waoneshe washiriki slaidi mbili zinazofuata (ya 8&ya9) za PPT, zinazoelezea ni nini mchoro wa mlima na mifano yake.

**PawaPointi** **PPT Kipindi cha 7**

- Watake washiriki waanze kuchora michoro yao ya  mlima. Wakati wakichora wafikirie tena maswali:
  - **Swali la 1**: Je, katika video hii aina zipi za vikwazo mbalimbali ambavyo watoto wanakabiliana navyo wakatii wa kwenda skuli?
  - **Swali la 2:** Kuna mifano gani katika video hii ambapo watu wengine au wanajamii walifanya kitu kusaidia watoto na kuondoa vikwazo walivyokuwa navyo?
- Waambie waoneshe katika milima hiyo (kwa kuchora au kwa maneno) vikwazo vya elimu mjumuisho walivyoviona katika video.
- Wakumbushe washiriki kwamba tulipojadili maana ya utetezi tuliona kwamba utetezi unahusisha kutafuta washirika wazuri na marfiki ili kujenga mitandao imara.
- Sasa watake washiriki waongeze katika milima yao ( kwa kutumia rangi nyengine) washirika, na mifumo ya usaidizi waliyoiona katika video.

## MAPUMZIKO YA CHAI

1 dk 30

### Maelekezo (yanaendelea)

- Baada ya chai washiriki waendelee na kazi zao za michoro ya milima.
- Sasa washiriki wafikirie kuhusu jamii zao wenyewe na kuongezea michoro na vikwazo vyengine vya elimu mjumuisho walivyoviona katika jamii zao.
- Wakumbushe washiriki walichojadili katika vikundi vyao katika kipindi cha vikwazo vya elimu mjumuisho siku iliyopita na aina mbalimbali za vikwazo ambavyo ni muhimu kuvifikiria. Video ilizingatia vikwazo vinavyowakabili wanafunzi kufika skuli tu lakini kuna vikwazo vyengine kadhaa ambavyo wanakabiliana navyo mara baada ya kufika skuli kama vile vikwazo vya ushiriki katika mchakato wa kujifunza darasani.
- Maelekezo haya pia yapo katika PPT ya 11.
- Baada ya washiriki kuonesha vikwazo vyengine katika michoro yao, waambie kuwa sasa waongeze (kwa rangi tofauti) washirika na mifumo ya usaidizi iliyopo katika jamii zao ambayo wanahisi ni muhimu katika kukabiliana na vikwazo vya elimu mjumuisho ambavyo wameviweka katika mchoro.
- Baadaye mtake mwakilishi wa kila kikundi kubandika kazi yao ukutani.
- Waambie washiriki wafanye ‘matembezi ya ukumbini’ waangalie kazi zao zilizopo katika kuta.
- Wakumbushe washiriki kusaidiana kwa kusoma kwa sauti na kuelezea michoro yao kwa wale ambao hawaoni au hawawezi kusoma.

## Shughuli ya 7.2 (iv): KUCHUKUA HATUA kushughulika vikwazo vya elimu mjumuisho na kuimarisha msaada

1 Dakika 60

### Maelekezo

- Wakumbushe washiriki kwamba sehemu ya tatu ya utafiti tatuzi ni kuhusu kuchukua HATUA -yaani kufanya jambo ili kuleta mabadiliko unayotaka kuayaona ( unaweza kuwaonesha tena Slaidi ya 5).
- Waeleze washiriki kwamba watafanya sehemu ya 'hatua' . Wataigiza hali halisi ambapo watu wanachukua hatua kuleta mabadiliko.
- Waeleze washiriki kuwa watafanya igizo-dhima litakalohusu kuchukua hatua kushughulikia vikwazo vya elimu mjumuisho katika jamii.

**Kitini 7.2** — **Igizo-dhima: Kushughulikia vikwazo vya elimu m jumuisho (kitini)**

### Kujitayarisha kwa ajili ya igizo

- Soma maelezo ya igizo-dhima kuhakikisha kwamba kila mmoja anajua kitu kinachoendelea katika igizo-dhima.
- Mpe kila mshiriki nakala ya kitini kinachoelezea igizo-dhima.
- Kisha waombe washiriki kujitolea kwa jukumu ambalo wangependa kuigiza.
- Mara baada ya washiriki kuamua nafasi wazopenda kuigiza, waambie kila mtu afikirie peke yake uzowefu alioupata uliopelekea kuwa na mitazamo na imani walizonazo kuhusu elimu mjumuisho. Hii itasaidia katika wakachosema katika igizo-dhima.
- Wakumbushe 'wanajamii' kufikiri kuhusu aina maswali ambayo wangependa kuuliza ikiwa watapiga simu katika kipindi cha redio.
- Mwambie kila mmoja kwamba ingawa kitini kinaeleza kuhusu igizo-dhima litakavyokuwa, washiriki wanaweza kuongezea vitu vipya kama wakipenda na wanaweza kutafsiri dhima zao jinsi wanavyopenda.
- Lengo ni kuwa kila mmoja aweze kufurahia shughuli hii.
- Kipange chumba kiwe kama kituo cha redio na waweke waigizaji wote katikati katika muundo wa nusu duara.

- Baada ya kutayarisha chumba, anza igizo na waambie washiriki kwamba igizo lao litachuka kiasi dakika 20.
- Baadhi ya maelekezo ya kuwakumbusha washiriki yapo pia katika PPT 12

## Wakati wa igizo-dhima

- Ukiwa kama mwezeshaji unaweza kukaa nyuma na kufurahia igizo. Hata hivyo, unaweza pia kihitaji kuwashajiisha 'wanajamii' to kupiga simu, au hata kuigiza kama mwanajamii wewe mwenyewe na kuuliza swali kusaidia kuamsha mazungumzo katika mwelekeo maalum au kusaidia kufafanua baadhi ya mambo.

## Baada ya igizo-dhima

- Baada ya kukamilika kwa igizo-dhima waite washiriki wakae sehemu zao na wajadili na kubadilishana mawazo juu ya maswali yaliyomo katika kitini
- Wakumbushe washiriki kwamba katika warsha hii hakuna majibu sahihi na yasiyo sahihi na daima ni vyema kuwa na mawazo na maoni tofauti. Mawazo na maoni ya kila mshiriki ni muhimu na yatathaminiwa.
- Washukuru wote kwa kushiriki.
- Eleza kwamba katika kipindi kinachofuata tutaanza kufikiria kuhusu yale tuliyojifunza kuhusu utetezi na jinsi gani tutakavyofanya utetezi katika jamii zetu

# Kipindi cha 8: Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho katika jamii

**Ujumbe muhimu**

- Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho
  - Kupinga mitazamo hasi na imani hasi
  - kupeana taarifa na mifano chanya
  - Kuwasaidia watu kuelewa kitu fulani tofauti ili ilete maana kwao
- Hatuwezi kubadili mitazamo na imani hasi za watu wengine. Tunaweza kubadilidsha mitazamo na imani zetu wenyewe. Kuelewa kitu kinachojenga mitazamo yetu wenyewe kutasaidia kuhoji mitazamo hasi na kutaimarisha mitazamo chanya kuelekea elimu mjumuisho kwa wengine.
- Kwa hivyo, kuwa watetezi wa elimu mjumuisho pia kuna maana ya kuwa ni wakala wa mabadiliko ambapo tutafanya kazi ya kuhoji mitazamo na imani hasi  na kuimarisha mitazamo na Imani chanya.

## Maelezo ya mwezeshaji

- Kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho kunhusisha zaidi ya kuwaambia watu elimi mmjumuisho ni nini. Kunahususha pia kuhoji mitazamo na imani hasi na  kuwasaidia watu kuelewa vizuri zaidi maana ya elimu mjumuisho na kwa nini ni muhimu.
- Ili kuekeleza hili, tunahitaji kujua vizuri zaidi asili ya mitazamo na imani zetu. Tunaweza kufanya kwa kutafakari ni nini kilichotengeneza mitazamo na imani  zetu wenyewe na kitu gani kinapelekea mabadiliko.
- Mitzamo na Imani zetu zinatokana na mchanganyiko wa uzowefu wetu na mambo tuliyjifunza, aghlabu kwa kipindi kirefu]
- Kwa hivyo, kushawishi mabadiliko chanya  katika mitazamo na imani za watu, kunachukua muda mrefu na kamwe haiwezi kuwa kwa mazungumzo ya mara moja, au kipindi kimoja cha redio au shughuli moja ya utetezi. Tukiwa kama ni wakala wa mabadiliko (watetezi)ni jukumu letu kupanda mbegu za mabadiliko na kujenga mazingira ambayo yatawezesha mabadiliko kutokea.

### Katika kipindi hiki washiriki

ü Watachunguza chanzo cha mitazamo na imani na kitu gani kinakuza mitazamo na imani hizo

ü Watatafakari juu ya mitzamo na Imani zao na kitu gani kimekuza mitazamo na imani zao ,

ü Watajifunza kuhusu njia chanya za kubadilisha mitazamo na imani na na kujenga uwelewa mpya wa elimu mmjumuisho katika jamii

## Shughuli ya 8.1: Mitazamo na imani zinatokea wapi?

1 Dakika 25

### Maelekezo

- Watake washiriki wafikirie nyuma katika Kipindi cha 3 ambapo tulizungumzia ubaguzi
- Wakumbushe kwamba walitakiwa kukumbuka wakati walipopata uzowefu wa ubaguzi. Moja kati ya maswali waliyotakiwa kuyafikiria ni:

**Kwa nini unadhani watu waliokubagua walifanya hivyo?**

- Waulize kama wanakumbuka baadhi ya sababu za ubaguzi.
- Chukua baadhi nya mawazo kutoka kwa washiriki. Baadhi ya sababu tulizozizungumza katika kipindi cha 3 zilikuwa:
    - **Woga/ hofu**
    - **Mitazamo hasi**
    - **Kutokuelewa au kukosa kuwa na taarifa sahihi**
    - **Uzowefu mbaya**
- Wakumbushe washiriki kwamba tulijadili 'mzunguko wa ubaguzi' na kujifunza namna ubaguzi unavyotokea kwa sababu ya mitazamo ya kibaguzi ambayo watu wanaweza kuwa nayo kwa watu wengine au vikundi vya watu wengine (mf. Wakimbizi). Mitazamo hii inaweza kuwafanya watu kuwa na tabia ambazo zinapelekea ubaguzi.
- Waambie washiriki kwamba mitazamo inaweza kuwa chanya au hasi.Mitazamo inaweza kupelekea ubaguzi. Lakini pia inaweza kupelekea


watu wakahoji ubaguzi na kuwa na harakati zinazochangia kufanya kila mtu kupata haki na rasilimali sawa.

- Waambie washiriki kwamba katika kipindi hiki tutatafakari kuhusu ni wapi mitazamo inakotokea ili tuweze kuelewa vyema kinachoweza kuelimisha na kujenga mitazamo jumuishi katika jamii. Pia tutatafakari kuhusu njia zenye ufanisi zaidi za kuipinga mitazamo yoyote hasi juu ya elimu mjumuisho na kuimarisha mitazamo chanya.
- Onesha PPT 8

**PawaPointi** **Slaidi ya 1 ya PPT ya Kipindi cha 8: Mitazamo na imani inatokea wapi (maduara ya mitazamo)?**

- Unaweza pia kuchora mchoro huu katika flipchati

## Mitazamo na Imani kuhusu elimu mjumuisho inatokea wapi?




[Maelezo ya picha: picha inaonesha maduara mawili yaliyoingiliana. Katika duara la upande wa kushoto inasema ‘ uzowefu( kilichotutokezea)’ Katika upande wa kulia, inasema ‘maarifa(kile tulichijifunza)’. Katika sehemu ya katikati yalipoungana maduara, inasema ‘ mitazamo & imani (kile tunachofikiri kuhusu vitu tunavyoviamini’ ]

- Hakikisha kwamba kila mtu ana karatasi nyeupe ya A4
- Waambie ( au msaidizi wake) wachore maduara mawili yanayopishana / yanayokatisha katikati kama ilivyo katika slaidi ya PPT. Maduara yawe makubwa ili waweze kuandika ndani yake.
- Chora seti yako mwenyewe katika flipchati ( utaitumia hii kuwaonesha washiriki kitu cha kufanya
- Waambie wayaandike maduara kama ilivyo katika PPT
- Hakikisha kwamba kila mtu ana kalamu tatu za rangi tofauti
- Kisha waambie washiriki wakumbuke katika kipindi cha 3 na wakati walipokumbuka walipofanyiwa ubaguzi
- Waambie waandike kwa mojawapo ya kalamu za rangi katikati ambapo maduara yanapishana kitu gani wanadhani ni mtazamo au imani gani muhimu zaidi iliyopelekea mtu huyo kufanya ubaguzi
- Waoneshe washiriki namna ya kufanya hivi kwa kuchora kuhusu uzowefu wako mwenyewe wa kubaguliwa na uandike mtazamo au imani hiyokatika flipchati.
- Baadhi ya mifano ni kama vile:
  - Ni muhimu zaidi kwa watoto wa kiume kwenda skuli kuliko watoto wa kike
  - Wanawake wanapaswa kuwa kimya kuhusu siasa
  - Watu wenye ulemavu hawawezi kushughulikia fedha zao
  - Watu wa nchi nyengine za Afrika Mashariki wanazichukua kazi zetu
- Waambie washiriki wafikirie **tukio moja** ( lililotokea) ambalo lingeweza kuchangia katika mtazamo huo. Waambie waandike tukio hilo **katika kalamu ya pili ya rangi** katika duara la ‘ uzowefu’.
- Waoneshe washiriki jinsi ya kufanya hivi kwa kuandika mfano wa tukio hilo ukijitolea mfano wewe mwenyewe.
- Waambie washiriki wafikirie jambo ambalo mtu/watu **walijifunza** skuli ambalo lingeweza kupelekea mtazamo huo. Waombe washiriki waandike hili katika duara la ‘ maarifa’ kwa kutumia **kalamu ya tatu ya rangi**.
- Waoneshe washiriki jinsi ya kufanya hivi kwa kuandika kitu ambacho kinaweza kuwa wamejifunza kuhusiana na mfano wako mwenyewe.

- Baada ya kila mmoja kumaliza kuandika mtazamo/imani, uzowefu na maarifa katika karatasi yake, waambie kila mmoja apeane na mshiriki aliyekaribu naye au wajadili katika vikundi vidogo vidogo.
- Baada ya kila mmoja kupata nafasi ya kupeana na mwenziwe/ wenziwe kazi waliyofanya , waulize washiriki maswali yafuatayo:
  - Kuna yeyote anayetaka kutoa maoni kuhusu shughuli hii?
  - Ilikuwa ni rahisi kiasi gani kujaribu kufikiria kuhusu mambo yaliyochangia mitazamo na imani za watu?
- Wakumbushe washiriki kuwa kipindi hiki kilihusu kuanza kufikiria mitazamo na imani na wapi zinakotokea. Pia kilikuwa kinahusu kukumbuka kuwa mitazamo na imani vina mchango muhimu katika ubaguzi, hivyo tunahitaji kuelewa ni wapi vinakotokea ili kuweza kupinga ubaguzi.
- Baada ya kumaliza majadiliano, waambie washiriki wabandike maduara yao ukutani.

## Shughuli ya 8.2: Kuelewa mitazamo na imani zetu wenyewe na za watu wengine

[1] Dakika 50

### Maelekezo

- Kabla ya kipindi tayarisha **'mabango ya vichwa vy habari'** katika karatasi za A3. Kila bango liwe na moja kati ya vichwa vya habari vya magazeti na wabandike kichwa cha Habari katika karatasi hiyo. Angalia **Kielelezo 8.1**
  - **Mwalimu mkuu anamrejesha mtoto wa kike nyumbani baada ya kugundulika kuwa ni mjamzito!**
  - **Wanajamii wanampiga kijana wa kiume kwa wizi**
  - **Wazazi wanaandamana baada ya skuli kuwakubali watoto ambao wana changamoto ya akili , wakijiteteta kwamba viwango vya skuli vitaporomoka**
  - **Walimu wanapinga sera ya kupiga marufuku matumizi ya bakora . Wanasema ni muhimu katika kuhakikisha nidhsmu madarasani!**

**Kielelezo 8.1** **Vichwa vya Habari vya magazeti**

- Tengeneza vipande vipana vya karatasi kwa kukata karatasi ya A4 vipande viwili. **Wape kila kikundi bango moja la kichwa cha habari** pamoja na vipande vipana vya karatasi
- Weka sanduku/boksi mbele ya darasa
- Waambie  washiriki wajadili katika vikundi mabango yao ya vichwa vya habari. Waambie waandike kwa kalamu ya rangi ya **BLUU** katika vipande vipana vya karatasi **MTAZAMO** wowote au **IMANI** ambazo wanafikiria zingeweza kumshawishi mwalimu mkuu, jamii, walimu au wazazi kuchukua hatua (dk 10) (kipande cha karatasi).
- Baada ya kumaliza waambie vikundi sasa watumie kalamu ya rangi ya **KIJANI** (au rangi nyengine) kuandika katika kipande kipana cha karatasi **UZOWEFU** au **KITU ALICHOJIFUNZA** ambacho kingeweza kushawishi mitazamo hii au imani (kiasi dk 10).
- Sanduku lifuatalo linatoa baadhi ya mitazamo, imani, uzowefu na ujifunzaji ambazo washiriki wanaweza kuzitaja wakati wa mijadala yao. Tumia sanduku hili kama ni rejea na kutoa mifano ikiwa washiriki wamekwama na wanahitaji usaidizi wa mawazo. Pia wanaweza kuja na mawazo yao ambayo hayamo ndani ya boksi hapo chini na n

**Mwalimu Mkuu amrudisha mwanafunzi nyumbani kutoka skuli baada ya kugundulika ni mjamzito!**

**Mitazamo/Imani:** Wanafunzi wajawazito ni ushawishi mbaya–wanaweza kuwashawishi wengine kupata ujauzito na hivyo hawapaswi kukaa darasani; wanafunzi wajawazito hawawajibiki na hawastahili kuwepo skuli. Watoto wa kike wanapaswa kuwa bikra wanapoolewa; kufanya ngono kabla ya ndoa ni makosa; ikiwa mtoto wa kike atapata ujauzito kabla ya kuolewa ni lazima ajifunze kutokana na makosa yake na kukubali matokeo yake.

**Uzowefu:** Mwalimu mkuu ana mtoto wa ndugu/kaka/dada yake ambaye amepata ujauzito akiwa bado yuko skuli; mwalimu mkuu anashinikizwa na jamii yake kukomesha mimba za utotoni katika jamii hiyo.

**Kujifunza:** Katika skuli tunajifunza kwamba ngono nje ya ndoa ni makosa; katika familia yangu nilijifunza kwamba ni lazima uadhibiwe ikiwa utafanya makosa.

**Wamshambulia kijana wa kiume kwa wizi!**

**Mitazamo/Imani:** Kijana huyo ni lazima afundishwe adabu; Jamii ina haki ya kuchukua sheria mikononi; Wizi ni uhalifu na lazima aadhibiwe; vijana wanajifunza kwa kupigwa tu.

**Uzowefu:** Uhalifu ni wa kwango cha juu katika jamii na polisi hawakufanya lolote wiki iliyopita wakati mzee mmoja katika jamii alipoibiwa.

**Kujifunza:** Katika kikundi changu cha vijana nilijifunza kwamba ni muhimu kumwadhibu kijana anapofanya kosa kwa sababu hivi ndivyo wanvyojifunza

**Wazazi waandamana baada ya skuli kuwapokea Watoto wenye ulemavu wa akili wakisema kwamba viwango vya skuli vitashuka**

**Mitazamo/Imani:** Watoto wneye ulemavu wa akili wasiruhusiwe kuja skuli, wawekwe nyumbani au wapelekwe katika skuli maalum.Skuli hii ina sifa kubwa na Watoto watasumbuka ikiwa watalazimika kubakia nyuma kwa sababu ya Watoto wenye mahitaji maalum; tulitoa nguvu zetu katika kujenga skuli hii na hii ni skuli yetu. Watoto wetu hawapaswi kuwa duni.

**Uzowefu:** Wazazi wawili wa watoto wenye ulemavu wa akili walilalamika kuwa kuna watoto wengine ambao wanawakebehi Watoto wao na hivyo Watoto hawana furaha). Mwalimu mkuu aliwaadhibu watoto wa skuli nzima na akaakhirisha siku ya kwenda matembezi waliyokuwa wakiitarajia.

**Kujifunza:** Nilijifunza kutoka kwa wenzangu kazini kwamba watoto wenye ulemavu wa akili hawawezi kujifunza mambo mengi. Rafiki yangu anasema kuwa walimu huambiwa kufanya kila kitu kuwa rahisi kwa watoto hao na watoto wengine hulipinga hilo na pia hawajifunzi.

**Walimu wapinga sera kuhusu kukomesha adhabu ya bakora – wanasema ni muhimu kudhibiti nidhamu wakiwa darasani**

**Mitazamo/Imani:** Bakora ndio njia pekee itakayowafanya wanafunzi kuzingatia masomo yao nio kujifunza; hakuna tatizo lolote kutumia bakora kwa mtoto; Ikiwa skuli zitaacha kutumia bakora, wanafunzi wataacha kuwaheshimu walimu.

**Uzowefu:** Nilipigwa skuli na hakuwa kitu kwangu; Nilijaribu kutumia njia nyengine za nidhamu na kwa haraka haraka

**Kujifunza:** Nilijifunza katika familia yangu kwamba bakora ni njia nzuri ya kuwafanya watoto kuwa na adabu; Nilijifunza kutoka kwa wenzangu katika

Chuo cha ualimu kuwa wakati mwengine ni sawa kutumia bakora kwa sababu.

- Wakiwa tayari waambie vikundi wabandike mabango yao ya vichwa vya habari ukutani pamoja na vipande vya karatasi vipana kuvizunguka (dk 5).
- Watake kila mmoja kuzunguka katika chumba cha warsha waangalie mabango yao ya vichwa vya habari na kile walichokiandika(dk5). Waambie warudi wakakae katika nafasi zao baada ya kuangalia mabango hayo.
- Waambie washiriki kwamba sasa tunataka kufanya jambo ambalo litakuwa gumu kwa sababu inatubidi kuwa **waaminifu** sana. Mtake kila mshiriki kuchukua kipande kipana cha karatasi na kuandika (kunakili) mtazamo wowote au imani yoyote kutoka ukutani ( iliyo katika rangi ya **BLUU**) ambayo wanakubaliana nayo, au waliyokuwa wakikubalina nayo zamani. Hapa utahitaji kutoa mfano wa jambo ambalo ni la ukweli kwako wewe. Kwa mfano, '' Nilikuwa nikiamini kuwa ni sawa kuwafundisha nidhamu watoto kwa kuwapiga bakora na ilisaidia kuwafanya wazingatie na wajifunze''. Waambie washiriki kuwa wanaweza kuzungukazunguka katika chumba cha warsha kama wanataka huku wakifikiria nini cha kuandika katika karatasi yao mpya.
- Waambie waikunje karatasi katika sehemu mbili na kisha waiingize katika boksi lililowekwa mbele darasani. Waambie kwamba walichokiandika katika karatasi hiyo ni siri na wasimwambie mtu mwengine kile walichokiandika.
- Baada ya kila mmoja kuingiza karatasi yake katika boksi, zichanganyechanganye vizuri na kisha umpe kila mshiriki karatasi moja. Waambie kila mmoja akabandike karatasi aliyopewa karibu na mtazamo au imani ukutani.
- Wakimaliz waambie warudi kukaa katika sehemu zao. Kwa ufupi waeleze washiriki wasioona ni wapi zilikobandikwa karatasi mpya ili waweze kuelewa zimewekwa karibu na mitazamo au imani zipi.
- Waulize washiriki iwapo wangependa kusema chochote kuhusu shughuli hii. Baadhi ya maswali ambayo unaweza kuuliza ili kuamsha mjadani ni:
    - Je, shughuli hii imekusaidia kuelewa vizuri zaidi ni wapi mitazamo au imani zinakotokea?
    - Unafikiri i muhimu kuelewa ni wapi mitazamo na imani zinakotokea ikiwa tunataka kushawishi mabadiliko katika elimu mjumuisho?

- Unafikiri ni muhimu kutafakari juu ya mitazamo na imani zetu wenyewe ikiwa tunataka kujaribu kushawishi mabadiliko ya mitazamo na imani za watu wengine?

- Onesha Slaidi ya 2 katika PPT ya 8 na wakumbushe washiriki kuhusu mambo muhimu tunayojifunza katika kipindi hiki.

**PawaPointi** **PPT ya Kipindi cha 8, Slaidi ya 2: Ujumbe muhimu.**

- Wakumbushe washiriki kwamba huu ni **ujumbe muhimu** kutoka katika kipindi hiki
  - Ni muhimu kukumbuka kwamba mitzamo na imani ya mtu inatokea sehemu fulani.
  - Hujengwa kutokana na UZOWEFU wa mtu na kutokana na YALE ALIYOJIFUNZA (skuli, nyumbani katika familia,kutoka kwa marafiki zao n.k.)
  - Kuelewa matukio haya na kutambua mambo ambayo mtu amefundishwa kunatusaidia kuelewa mahali ambapo mitazamo hasi na imani hasi kuhusu elimu mjumuisho zinakoweza kutokea na hiyo hutusaidia kumwonea huruma /kumuelewa mtu huyo, hata kama hatukubaliani naye.
  - Kuelewa mambo yanayojenga mitazamo na imani zetu wenyewe pia hutusaidia kuelewa kwanini watu wengine huwa na fikra au imani tofauti na zetu.

## Shughuli ya 8.3: Kushawishi mitazamo na kujenga uwelewa mpya

1 Dakika 45

### Maelekezo kwa mwezeshaji

- Waeleze washiriki kwamba sasa tunataka kuzungumza kuhusu kushawishi na kupinga mitazamo hasi na mambo yanayotusaidia kuweza kufanya hivyo.
- Waambie washiriki wakae wawiliwawili ( waambie wachague mtu ambaye hadi sasa bado hawajafanyakazi pamoja)

- Hakikisa wanakaa vizuri kwa kuacha nafasi ya kutosha baina yao ili waweze kuzungumza vizuri.
- Sasa waambie wafikirie wakati wa zamani walipobadilisha mtazamo au imani kuhusu jambo lolote ( inaweza kuwa kubwa au dogo)
- Waambie wajadiliane KWANINI walibadili mitazamo yao –(hii inaweza kuwa jambo Fulani lililotokea, jambo ambalo waliambiwa na mtu mwengine, jambo walilosoma au walilolisikia au jambo lolote ambalo lilisababisha wao kubadili mitazamo yao)
- Mpe kila mtu muda wa kutosha kutafakari hayo na mwenziwe (kiasi dk10)
- Waulize iwapo kuna mtu anataka kueleza chochote kwa washiriki kuhusu majadiliano yake na mwenziwe(dk 5) Baadhi ya maswali ya kuamsha mjadala yanaweza kuwa:
  - o Je, ilikuwa vigumu kufikiria kuhus jambo lililobadilisha mtazamo au imani yako?
  - o Je, ni jambo gani lilikusaidia kubadilisha mtazamo au imani yako?
- Baada ya kumaliza kutafakari juu ya majadiliano haya waambie washiriki kuwa sasa tutafanya igizo-dhima wakiwa katika jozi zao (wawiliwawili).
- Elezea kwamba watafanya igizo-dhima kuhusu majadiliano waliyofanya watu wawili wawili – mtu mmoja kutoka katika Jumuiya za Watu wenye Ulemavu na mtu anayeshughulika na moja ya TRRT2
- Mwezeshaji awatake kila jozi kuonesha igizo-dhima kwa kutumia moja kati ya mikutano ifuatayo. Elezea kwamba katika kila mkutano mjumbe wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu:
  - o Atajaribu kuelewa **ni wapi mtazamo wa mtu mwengine unakotokea** uliopelekea kufanywa kwa tukio lililoelezwa katika kicwa cha habari cha gazeti
  - o Atajaribu kuhakikisha kwamba huyo mtu mwengine **hajisikii kuhukumiwa** na anaweza kuelezea maoni yake(**uelewa)**
  - o Atajaribu kumshawishi mtu mwengine kubadilisha fikra zake ili awe huru kuanza kufikiria tofauti kuhusu jambo alilolifanya **(ushawishi).**

    **Mkutano wa 1**: Baina ya mwalimu mkuu aliyemrejesha mtoto mwenye ujauzito nyumbani na mwanachama wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu katika eneo ambalo skuli ipo.

**Mkutano wa 2:** Baina ya mwanajamii ambaye alishiriki katika kumwadhibu kijana aliyekamatwa akiiba na pia ni mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu katika jamii

**Mkutano wa 3:** Baina ya mwenyekiti wa jumuiya ya wazazi kutoka katika skuli ambayo imepokea wanafunzi wenye ulemavu wa akili hivi karibuni na pia mwanachama ni mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu katika jamii

**Mkutano wa 4:** Baina ya mwakilishi wa chama cha walimu ambaye amepinga sera kuhusu adhabu ya bakora na pia ni ni mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu katika jamii hiyo hiyo.

- Onesha **Slaidi ya 3 ya PPT 8** kiuwakumbusha washiriki kuhusu stadi kuu za **kusikiliza, kuelewa** na **kushawishi**

**PawaPointi**

**Slaidi ya 3 ya PPT ya Kipindi cha 8: Stadi muhimu za kukuza uwelewa**

- Unaweza pia kuziandika stadi hizi katika flipchati
- Waeleze washiriki kuwa watakuwa na dk 20 kwa ajili ya igizo-dhima.
- Baada ya dk 20 washiriki wote watakaa tena pamoja.
- Watake washiriki sasa watafakari juu ya igizo-dhima kwa kuwauliza maswali yafuatayo (kiasi dk 7):
  - Kama ungelikuwa ni mwalimu mkuu, mwanajamii, mzazi/mwanachama wa Jumuiya za Watu wenye Ulemavu, je kuna jambo lolote ambalo mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu alikwambia au alifanya katika mkutano ambalo lilishawishi mabadiliko ya fikra zako katika njia chanya (ambayo ilifanikiwa)
  - Kulikuwa na jambo lolote alilokwambia au alilokufanyia lililokufanya ujisikie vibaya au kukufanya uwe na hasira ( ambalo halikufanikwa)?
  - Iwapo ungekuwa mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu ni kitu gani ilikiona kigumu zaidi katika mazungumzo yenu na mtu huyo?
  - Iwapo ungekuwa mwanachama wa Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu kulikuwa na kitu chochote ulichofanya au kusema ambacho kilikufanya ujihisi kuwa ulipiga hatua katika kukufanya ufikiri tofauti kidogo?

- o Je, kuna mambo mengine yoyote yaliyojitokeza katika maigizo-dhima yenu ambayo mnadhani ni muhimu kuyatafakari katika majukumu yenu kama watetetzi wa elimu mjumuisho?

- Onesha Slaidi ya 4 katika PPT8 na pitia ujumbe muhimu

**PawaPointi** **PPT ya Kipindi cha 8, Slaidi ya 4: Ujumbe Muhimu**

- Taja mambo yafuatayo:
  - Hatuwezi kubadilisha mitazamo na imani za watu wengine. Tunaweza tu kupinga na kushawishi mawazo yao na kuwatengenezea fursa za kufikiri na kufanya mambo kwa njia tofauti. Fursa hizi hutokea kwa:
  - Kuonesha subira na uwelewa kuelekea mitazamo na imani zao (huruma)
  - Kupeana habari mpya (maarifa mapya)
  - Kuwatengenezea mazingira ya kupata uzowefu kwa njia tofauti na zile walizozizowea wakati uliopita ( uzowefu chanya)
  - Kupinga na kushawishi mabadiliko ya mitazamo na imani za watu kunachukua muda mrefu-kwa hivyo utetezi mzuri kuhusu elimu mjumuisho unahusisha kuwa ni wakala wa mabadiliko ambapo tunaendelea kufanyakazi ya kupinga mitazamo hasi kuhusu elimu mjumuisho na kujenga uwelewa mpya juu ya umuhimu wa elimu mjumuisho.

# Kipindi cha 9: Kutafakari kuhus kujifunza na uzowefu

**Ujumbe muhimu**

- Hali zenye changamoto au mazingira magumu yanaweza pia kuwa ni fursa kwa kujifunza na mabadiliko.
- Mashirikiano (kufanyakazi pamoja) tunaweza kupata masuluhisho bora zaidi katika changamoto zinazotukabili

## Maelezo kwa mwezeshaji

- Kipindi hiki kinawakaribisha washiriki kutafakari juu ya kile walichojifunza wakati wa warsha na kuongeza ujifunzaji wao katika Mto wa Maisha.
- Kipindi hiki pia kitawasaidia washiriki kutafakari na kubadilishana uzowefu ambao tayari wanao katika masuala ya elimu mjumuisho.
- Shughuli ya pili inatumia mkabala unaoitwa 'Uchunguzi wa kuthamini' ( Appreciative inquiry). Uchunguzi wa kuthamini ni ni mkabala wenye mtindo wa utafiti tatuzi ambao unatusaidia kuzingatia zaidi vipengele chanya katika maisha au kazi zetu, badala ya kuzingatia matatizo pekee. Mkabala huu hututia moyo kuona nguvu na fursa badala ya kuona changamoto na udhaifu tu, na kufikiria jinsi ya kujiimarisha kupitia mambo mazuri ambayo tayari tunayo. Mkabala kuthamini huchukulia kuwa kila hali ina mambo chanya ambayo yanaweza kuchunguzwa na kutumiwa kama msingi wa kujenga mambo mazuri zaidi.

### Katika kipindi hiki washiriki

ü Watatafakari kuhusu warsha hii na mambo waliyojifunza

ü Watabadilishana uzowefu walionao juu ya masuala ya elimu mjumuisho.

## Shughuli ya 9.1: Kupitia upya Mto wa Maisha

1 Dakika 45

### Maelekezo

- Watake washiriki wajadili katika vikundi kwa dakika chache wajikumbushe kuhusu maudhui ya warsha hadi sasa. Tumia slaidi 1-6 kusaidia kuanza mazungumzo
- Waambie watizame tena Mto wa Maisha, na waangalie zile kadi zao walizobandika katika sehemu za mto huo hapo kabla.
- Waambie washiriki wafanye kazi mmoja mmoja wachore au waandike kauli kuonesha walichojifunza katika warsha hii.
- Kisha wanaweza wakajadili michoro yao katika vikundi. Waeleze kwanini hiki kilikuwa ni kipindi muhimu cha kujifunza na ambacho hakitasahaulika.
- Waambie washiriki wakabandike michoro yao au kauli zao karibu na sehemu ya mwisho wa  warsha katika sehemu kuu za mto. Ikiwezekana, wapige mstari baina ya waliyojifunza na maswali ambayo walitumai warsha ingeyajibu mwanzoni mwa Mto wa Maisha. Wanaweza kutumia mstari uliokoza kuonesha mambo muhimu waliyojifunza vizuri, na mstari wenye nukta ili kuonesha pale ambapo walijifunza kitu lakino bado wana mashaka nacho.
- Waalike baadhi ya washiriki kuelezea wenzao kitu walichojofunza.

## Shughuli ya 9.2: ‘Maduara ya ushirikiano’

1 Dakika 60

### Maelekezo

- Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 4-5
- Onesha PPT Slaidi ya 1-4 ya Kipindi cha 9

**PawaPointi** **PPT ya Kipindi cha 9**

- Kisha onesha slaidi ya 7 na elezea maelekezo ya shughuli ya 'maduara ya ushirikiano', kama ifuatavyo:
  - Kila mtu afikirie kuhusu changamoto aliyo nayo katika kusonga mbele na harakati za utetezi wa elimu mjumuisho
  - Mtu wa kwanza atumie dakika 2-3 kuelezea changamoto yake kwa wanakikundi wenziwe.
  - Wenzake katika kikundi watakuwa ni watampa ushauri, mrejesho, na mawasiliano ya watu/ jumuiya zinazoweza kumsaidia juu ya changamoto hiyo. Pia watatoa uzowefu wao wenyewe katika kukabiliana na hali kama hiyo, na jinsi ya kugeuza changamoto kuwa fursa.
  - Mwisho, kikundi kibaini mafunzo muhimu waliyojifunza kutokana na kisa mafunzo hiki na ushauri uliotolewa (dakika 2-3).
- Sisitiza kwa washiriki kwamba wanakikundi wanaotoa ushauri ni lazima watoe ushauri chanya na wazingatie kutoa suluhisho na sio kuonesha huruma tu.
- Waambie washiriki kurudia mchakato huu hadi kila mmoja katika kikundi amepata nafasi ya kuelezea changamoto yake na kupata ushauri.
- Baadaye washiriki warudi kukaa pamoja waelezee mafunzo muhimu waliyoyapata kwa kuzingatia jinsi ya kubadilisha changamoto au tatizo kuwa fursa au suluhisho.



Kikundi cha washiriki wakati wa shughuli ya duara la ushauri nchini Zanzibar

[Maelezo ya picha: wanawake 8 na mwanamme mmoja wakiwa wamesimama kwa mduara. Wako nje. Mwanamke mmoja anaonekana akizungumza huku na waliobaki wanamwangalia na wanamsikiliza.]

## MAPUMZIKO YA CHAI

# Kipindi cha 10: Kujenga Uwezo wa Utetezi: kukusanya taarifa kwa ajili ya kujenga uwelewa

### Katika kipindi hiki washiriki:

ü Watatafakari dira yao ya elimu mjumuisho katika wilaya na jamii zao

ü Wataongezea juu ya kile walichokwishajifunza kuhusu utetezi na mitazamo ili kuelewa kwa nini ni muhimu kwanza kuangalia na kufikiria kuhusu mitazamo juu ya elimu mjumuisho katika jamii kabla hatujaanza kukuza uwelewa

ü Buni na anza kupanga mchakato wa kukusanya taarifa za wanachokijua na wanachofikiri watu katika jamii kuhusu elimu mjumuisho. Hii itakuwa hatua ya mwanzo ya kutoa elimu kuhusu elimu mjumuisho katika jamii ( Kujenga Uwezo wa Utetezi: Awamu ya 1)

## Shughuli ya 10.1: Kufikiria wakati ujao

1 Dakika 20

### Maelekezo

- Mtake kila mmoja kukaa vizuri katika kiti chake na kufumba macho. Ikiwa kuna yeyote ambaye hajisikii vizuri kufumba macho anaweza kuyaacha wazi ila ni vyema kujua kuwa unaweza kujenga picha vizuri zaidi kuhusu wakati ujao ukiwa umefumba macho.
- Soma taarifa ifuatayo kidogokidogo huku ukisita baada ya kila sentensi:

  ‘‘Huku ukiwa umefumba macho, pumua kwa kina. Fikiria umerudi katika wilaya yako baada ya muda fulani katika wakati ujao. Uko katika jamii yako pamoja na familia yako na wanajamii wenzako mnaofanya kazi pamoja. Fikiria kwamba wilaya yako imefanya mambo mengi ya kuunga mkono elimu mjumuisho kwa miaka mingi na kumekuwa na mabadiliko mazuri katika mambo mengi. Ni mifano gani ya mambo hayo uliyoyaona yamebadilika? Elimu mjumuisho inaonekanaje katika jamii yako? Elimu mjumuisho inaonekanaje katika skuli zilizoko katika eneo hilo? Tumia muda kiasi kufikiria mabadiliko haya na jinsi familia, watoto, vijana, wazazi na jamii kwa ujumla ilivyobadilika.  Kuna mifano gani na ushadi gani wa

maendeleo ya elimu mjumuisho unayoyaona? Unajisikiaje kuyaona mabadiliko yote haya?''

- Pumzika kwa dakika mbili kisha useme: '' Sasa utarudi hadi katika siku ya leo. Fumbua macho yako kidokidogo na zungusha macho yako kuangalia sehemu mbalimbali katika chumba cha warsha hii.''
- Waambie washiriki wakae kwa jozi (wawiliwawili) pamoja na mjumbe mwengine kutoka Jumuiya iliyo katika Wilaya yake. Wanaweza pia kukaa katika vikundi vya watu watatuwatatu. Ikiwa atabaki mshiriki mmoja peke yake baada ya wenzake kukaa kwa jozi au watatuwatatu, atajiunga na jozi au kikundi chochote.
- Katika jozi (au vikundi) waambie washiriki kutafakari kwa ufupi kuhusu shughuli ya kujenga taswira ya wakati ujao na wajadili maswali yafuatayo:
  - Ulifikiria mabadiliko gani katika skuli na jamii yako?
  - Ulijisikiaje kufikiria kuhusu mabadiliko hayo?
- Chukua majibu kutoka kwa mshiriki mmoja hadi wawili.

## Shughuli ya 10.2: Kupanga kwa ajili ya Kujenga Uwezo wa Utetezi (awamu ya 1): kukusanya taarifa kwa ajili ya kukuza uwelewa

**Ujumbe muhimu**

- Kabla ya kuanza kujenga uwelewa kuhusu elimu mjumuisho katika jamii, tunahitaji kwanza kukusanya taarifa kuhusu ni kitu gani wanajamii wanajua na kuelewa kuhusu elimu mjumuisho –tunaweza tukadhani tunajua hayo, lakini hatuwezi kuwa na uhakika.
- Hii ina maana ya kwamba tunahitaji ku CHUNGUZA mitazamo na imani zilizopo na KUFIKIRI kuhusu mitazamo na imani hizo –hii itatusaidia kuweza kujenga uwelewa wa elimu mjumuisho kwa ufanisi
- Kwa hivyo, tuahitaji KUCHUNGUZA na KUFIKIRI kuhusu mitazamo na imani katika jamii KABLA ya kuanza kazi ya kujenga uwelewa
- **Kukusanya taarifa** katika jamii kuhusu mitazamo na imani za watu kunahusisha kupanga kwa uangalifu ili kujitayarisha vizuri kwa kile tunachotaka kufanya.

### Maelezo kwa ajili ya mwezeshaji

- Kipindi hiki kitaongezea katika yale tuliyojifunza kuhusu mzunguko wa utafiti tatuzi ( chunguza, fikiri, chukua hatua) na kuhusu mitazamo.
- Ni muhimu kuelewa kwamba ingawa awamu ya 1 ya Kujenga Uwezo wa Utetezi kunahusu kukuza uwelewa katika jamii, kwanza tunahitaji kuelewa ni nini watu wanafikiri na kuelewa kuhusu elimu mjumuisho kabla hatujaanza kupanga kuhusu kujenga uwelewa
- **Kwa hivyo, hatua ya kwanza ya kujenga uwelewa au sehemu ya kwanza ya Mpango wa Utetezi ni kwenda katika jamii na kukusanya taarifa kuhusu ni nini watu wanafikiri na kuelewa kuhusu elimu mjumuisho.**
- Kipindi hiki kimekusudiwa kusaidia Jumuiya za Watu wenye Ulemavu kufikiri na kupanga jinsi ya kukusanya taarifa hizo
- Lengo ni kuziwezesha Jumuiya za Watu wenye ulemavu kuondoka katika warsha hii wakiwa na mawazo mazuri na hatua katika kupanga za kukusanya taarifa hizo.

### Katika kipindi hiki watashiriki:

ü Kuongezea katika waliyokwishajifunza kuhusu utetezi na mitazamo na kuelewa ni kwa nini ni muhimu kwanza kuchunguza na kufikiria kuhusu mitazamo juu ya elimu mjumuisho katika jamii kabla ya kuanza kujenga uwelewa kwa ufanisi

ü Kubuni na kuanza kupanga mchakato wa kukusanya taarifa kuhusu nini watu wanafikiri na wanajua kuhusu elimu mjumuisho

## Shughuli ya 10.2 (i): Kukumbuka kwa nini KUCHUNGUZA & KUFIKIRI ni muhimu

1 Dakika 10

- Waelezee washiriki kwamba sasa tutaangalia kwa pamoja kuhusu utetezi na duara la utafiti tatuzi pamoja na yale tuliyojifunza kuhusu mitazamo na imani
- Tutafanya kazi hii kwa hivyo tunaweza kuanza kupanga kazi yetu ya utetezi wa elimu mjumuisho katika jamii

- Katika kipindi hiki tutapanga kuhusu mambo tunayohitaji kufanya kabla ya kuanza kukuza uwelewa wa elimu mjumuisho katika jamii.
- Onesha Slaidi ya 1 ya PPT ya Kipindi cha 10.2

**PawaPointi** **slaidi ya 1ya PPT 10.2: Kupanga KUCHUNGUZA & KUFIKIRI kuhusu mitazamo & imani juu ya elimu mjumuisho**

- Waoneshe washiriki Slaidi ya 1 ( duara la utafiti tatuzi) ( au tumia picha ya duara la utafiti tatuzi) na wakumbushe washiriki kwamba:

**Kuwa mtetzi mzuri maana yake ni kwanza ni kuchunguza na kufikiri kabla ya kuchukua hatua**

- Sasa waoneshe washiriki Slaidi ya 2 (maduara ya mitazamo) (au tumia flipchati zenye maduara ulizozitumia katika kipindi cha 8).wakumbushe kuwa tuijifunza katika kipindi cha
- Sasa waoneshe **Slaidi ya 3 (kwa rangi ya manjano na wardi)** na elezea kwamba:

**Kabla ya kuchukua hatua ya kushawishi na kupinga mitazamo hasi kwa elimu mjumuisho na kuimarisha mitazamo chanya, tunahitaji:**

  - kwanza KUCHUNGUZA mitazamo na imani za watu katika jamii
  - na kisha KUFIKIRI kuhusu uzowefu na maarifa ambayo huenda yalichangia kuwepo kwa mitazamo na imani hizi.

- Waoneshe washiriki Slaidi ya 4 ambayo inauliza swali kubwa:

**VIPI tuna CHUNGUZA na KUFIKIRI kuhusu mitazamo na imani kuhusu elimu mjumuisho katika jamii?**

- Waeleze washiriki kwamba sasa tutajadili ni VIPI tunaweza kuchunguza na kufikiri kuhusu mitazamo na imani kuhusu elimu mjumuisho katika jamii.

## Shughuli ya 10.2 (ii): VIPI KUCHUNGUZA & KUFIKIRI kuhusu mitazamo na imani kuhusu elimu mjumuisho katika jamii

1 Dakika 80

- Waambie washiriki wakae kwa jozi.
- Hakikisha kuwa kila jozi ina karatasi 6 za A4
- Sema kwa washiriki kwamba sasa tutajadili jinsi ya KUCHUNGUZA na KUFIKIRI kuhusu mambo ambayo watu katika jamii wanajua kuhusu elimu mjumuisho pamoja na kuchambua mitazamo na imani zinahusu nini?
- Onesha Slaidi ya 5 (katika PPT) na watake washiriki kujadili swali lifuatalo wakiwa wawiliwawili.

**Je ni NINI sisi kama JUMUIYA YA WATU WENYE ULEMAVU tunaweza kufanya (hatua tunazoweza kuchukua) kukusanya taarifa kuhusu mambo wanayoyajua watu katika jamii yetu kuhusu elimu mjumuisho na ni ipi mitazamo na imani zao kuhusu elimu mjumuisho?**

- Watake washiriki wakiwa katika jozi zao wajadili swali hili na wakubaliane na hatua 3 ambazo Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu inaweza kuchukua katika kukusanya taarifa kuhusu kile watu wanachokijua na kufikiri kuhusu elimu mjumuisho
- Waambie waandike kila hatua katika karatasi ya A4
- Waambie kwamba waandike mawazo yao kwa maandishi makubwa.
- Wape kiasi dakika 20 kujadili swali hilo na waandike hatua zao 3
- Waambie wabandike karatasi zao ukutani baada ya kuandika mawazo yao.
- Baada ya jozi zote kuweka hatua zao ukutani, soma polepole hatua zote ambazo washiriki wameziandika.
- Waambie washiriki kwamba sasa unawataka wajadili hatua hizo zilizopo ukutani na waamue ni hatua ipi ambayo wao kama Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu wanataka kuichukua ili kukusanya taarifa katika jamii. Ongoza majadiliano kwa kuwauliza swali lifuatalo (Slaidi ya 6):

**Je, ni hatua ipi itatupa fursa bora zaidi kukusanya taarifa kuhusu ni nini watu katika jamii yetu wanafikiri na wanajua kuhu elimu mjumuisho?**

- Waache washiriki wajadiliane kuhusu jambo hili, lakini jaribu na hakikisha kwamba wanafikia makubaliano ili hatimaye iwe wazi ni hatua gani wanataka kuchukua. Wakumbushe kwamba tunachunguza hatua ambazo zitapelekea kuweza kukusanya taariza kwa ufanisi zaidi kuhusu kile watu wanachokijua na kufikiri kuhusu elimu mjumuisho ( sio kazi za utetezi zitakazokuza uwelewa–ndio kwanza tunakusanya taarifa)
- Baada ya kufikia makubaliano, andika vizuri katika flipchati: Hatua Yetu ( andika hatua iliyokubaliwa)
- Watake washiriki warudi katika jozi zao. Eleza kwamba sasa tutafikiri kwa uangalifu zaidi kuhusu hatua tuliyoichagua (hatua yetu) ili tuanze kupanga. Wape kila jozi nakala ya Karatasi ya Hatua.

**Kielelezo cha 10.2** **Karatasi ya Hatua ya kufikiria kuhusu hatua ya kukusanya taarifa**

- Onesha Slaidi ya 7 na watake kila jozi kujadili maswali yaliyopo katika slaidi. Watake waandike majibu yao katika Karatasi ya Hatua ambayo watayatumia baadaye. Haya hapa maswali katika slaidi:
  - o **Je, hatua hii itatupa fursa ya kusikiliza kwa umakini yale wanayoyasema watu (KUSIKILIZA)?**
    - I. Kama ndio, ni vipi?
    - II. Kama hapana, ni kitu gani tukibadilishe katika hatua hii ili tupate njia bora zaidi ya kuwasikiliza watu katika jamii?
  - o **Je, hatua hii itatuwezesha kuwafikia watu katika jamii(MITAZAMO NA IMANI MBALIMBALI)?**
    - I. Kama ndio, ni vipi?
    - II. Kama hapana, ni kitu gani tukibadilishe katika hatua hii ili tupate njia bora zaidi ya kuwasikiliza watu katika jamii?
  - o **Je tutahitaji ujuzi/stadi gani katika kutekeleza hatua hii (UWEZO WETU)? (katika Slaidi ya 8)**
    - I. Je, tuna ujuzi/stadi hizi katika Jumuiya yetu ya Watu wenye Ulemavu
    - II. Kama ndio, vipi tutahakikisha tunatumia vizuri ujuzi/stadi hizi ?
    - III. Kama hapana, je, tunaweza kutafuta njia ya kuzipata au tunahitaji kubadilisha hatua hii na kuchukua hatua nyengine ambayo tuna ujuzi/stadi zinazohitajika?

- Baada ya washirki kupata nafasi ya kujadili kila swali na kuandika jawabu zao (dk 30), waambie wakusanyike tena wote kwa pamoja.
- Waambie washiriki wafikirie kidogo na waseme iwapo kuna kitu chochote wangependa kukibadilisha kuhusu hatua waliyokubaliana. Ikiwa watashauri mabadiliko yoyote waambie waeleze kwa nini wanataka mabadiliko hayo na andika sababu hizo kwa makini katika flipchati.
- Jaribu kuwaambia washiriki wafikie muafaka kuhusiana na mabadiliko yatakayohitaji kufanyika katika hatua yao waliyokubaliana.
- Mwisho wa majadiliano haya hakikisha unanakili vizuri maafikiano yao ili kila mmoja aelewe vizuri kuhusu hatua ambayo Jumuiya imepanga kuchukua katika kukusanya taarifa kuhusu kile ambach watu katika jamii wanafikiri na wanaelewa kuhusu elimu mjumuisho.

## Shughuli ya 10.2 (iii): Kupanga hatua zinazofuata za kukusanya taarifa

1 Dakika 40

- Kabla ya kuanza shughuli hii hakikisha kwamba umenakili Mpango wa Chunguza & Fikiri (katika Slaidi ya 11) katika flipchati (unaweza kuhitaji zaidi ya karatasi moja).
- Waeleze washiriki kwamba sasa mtafanyakazi kama Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu kupanga hatua za baadae kuhusu hatua ya kukusanya taarifa tuliyokubaliana nayo.
- Onesha Slaidi ya 10 ( maelezo ya hatua zinazofuata za Ujenzi wa Uwezo wa Utetezi : Awamu ya 1 (pia hapa chini)

**Hatua zinazofuta**

- Tekeleza Hatua 1,2&3(Juni hadi Julai 2021)
  - Kamilisha mpango wetu
  - Kwenda katika jamii na kuanzisha hatua yetu ya kukusanya taarifa
  - Kujitayarisha kukusanya taarifa (vifaa vya utafiti)
- Tekeleza Hatua ya 4 (Julai 2021)
  - Kukusanya taarifa zetu
- Tekeleza Hatua ya 5 ( Julai-Agosti 2021
  - Kuweka taarifa zetu zote pamoja
- Tekeleza Hatua ya 6 (Agosti 2021)
  - Kufikira kuhusu kile tulichokipata na kujitayarisha na warsha inayofuata

- Pitia hatua mbalimbali pamoja na washiriki wote ili iwe wazi kwa kila mmoja juu ya hatua kuu ambazo wanataka kuzichukua baada ya warsha na muda uliopo kuelekea katika warsha itakayofanyika mwezi wa Septemba.
- Waoneshe Slaidi ya 11- **Mpango wa CHUNGUZA & FIKIRI (** na katika flipchati**)**
- Waeleze washiriki kwamba sasa tutafikiri zaidi kidogo kuhusu hatua yetu tuliyoipanga ya kukusanya taarifa na tutatumia **Mpango wa CHUNGUZA, FIKIRI & Panga.**
- Uliza iwapo kuna mshiriki ambaye angependa kuandika yale yote yaliyokubalika katika mpango ulio katika flipchati
- Sasa pitia kila hatua na kwa kila hatua watake washiriki wajadili na kuamua kuhusu maswali haya. (Waelezee washiriki kwamba ingawa mnafikiria kuhusu hili sasa hivi, inaweza kubadilishwa baada ya mpango kumalizika)
  - **KITU GANI tutafanya kutekeleza hatua hii**?( hapa ni muhimu kufikiria mambo yanayotakiwa yafanyike)
  - NANI atachukua dhamana? ( hapa ni muhimu kufikiria kuhusu ni mtu gani sahihi/bora katika Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu achukue dhamana hii)
  - **HADI MUDA GANI tutakuwa tumefanya hili**? ( kumbuka tarehe za mwisho katka slaidi iliyopita – kuepuka tarehe kuingiliana.

- Kuna hatua 6 kwa hivyo toa kiasi dk 4 hadi 5 kwa kila hatua ( lakini kubali iwapo wengine watachukua muda zaidi ya uliotoa).
- Baada ya kufanyika mjadala kwa kila hatua, hakikisha kwamba mwandishi amenakili vizuri kila kilichosemwa katika flipchati.
- Baada ya kupitia hatua zote 6 na baada ya kunakiliwa katika flipchati yote yaliyosemwa, mshukuru kila mmoja kwa ushiriki wake na kwa mawazo yake.
- Angalia Mpango wa Chunguza, Fikiri& Panga na uliza iwapo kila mmoja ameelewa yale waliyoamuliwa. Ruhusu mshiriki yeyote kuuliza maswali iwapo wanayo.
- Mkumbushe kila mmoja kuhusu yaliyokubaliwa kwa Hatua ya 1.
- Waeleze washiriki kwamba timu ya wawezeshaji (Saida, Safia, Suleiman, Mohammed, Jecha na Anise) itakuwepo kuwaunga mkono na kuwasaidia katika kutekeleza mipango yao.
- Sema kwamba timu hiyo itakuwa inawasiliana nao kufuatilia mambo yanavyokwenda, na watakuwa wakiwapelekea nyenzo/ vifaa zaidi kuwasaidia katika mchakato wa ukusanyaji wa taarifa.

# Vielelezo na vitini

Moduli ya

1

# Kielelezo 2.1: Kujifunza kunaonekanaje?

## Picha kwa ajili ya majadiliano

Chapisha na ukate picha zilizopo kwenye kurasa zifuatazo zikiwa moja moja kabla ya kuanza kwa warsha, na weka seti moja ya picha katika kila kikundi cha washiriki. Maelezo yaliopo chini ya kila picha ni kwa ajili ya kukusaidia wewe kurejea wakati majadiliano yakiendelea. Hakikisha umeyaondoa maelezo hayo baada ya kuchapisha picha kabla ya kuwapa picha hizo washiriki.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

### Tunajifunza nini?

**Stadi za maisha:** Watoto hujifunza stadi muhimu za maisha kwa kufanya kazi za nyumbani Ni muhimu kwa watoto wa kiume na wa kike kushiriki katika utekelezaji wa majukumu haya ili kuondoa ubaguzi wa kijinsia.

**Msamiati, mashairi na mirindimo:** Kuimba pamoja ni namna nzuri ya kuwafunza watoto  misamiati, mirindimo na mashairi, pamoja na ubunifu.

**Kusikiliza mazingira:** (ndege anaimba dirishani) husaidia watoto kupenda mazingira jambo ambalo ni muhimu katika nyakati ambazo mabadiliko ya tabia nchi yanamuathiri kila mtu.




## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

### Tunajifunza nini?

**Msamiati na lugha:** Kusimulia hadithi, ziwe za kubuni au za kweli ni utaratibu mzuri kwa ajili ya kuwasaidia watoto kujifunza lugha, ubunifu na kutafakari kwa kujenga hoja.

**Kuwasikiliza wengine:** Kujifunza kupitia watu wazima na uzoefu walionao ni njia bora ya kujifunza. Huwawezesha watoto kuwapenda na kuwathamini watu waliomo katika familia zao na jamii.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

**Tunajifunza nini?**

**Stadi za maisha:** Kujifunza stadi za maisha kama vile jinsi ya kuotesha mimea ni muhimu sana kwa watoto. Watoto pia hujifunza jinsi ya kuvitunza viumbe hai – mmea, na kuuhudumia kila siku.

**Uvumilivu na utafiti:** Mimea hukua taratibu, watoto hujifunza uvumilivu na utafiti wakifuatilia ukuaji wa mmea

**Kujifunza kupitia wengine:** kujifunza kupitia kwa watu wengine katika familia au jamii wenye ujuzi ambao wewe huna.



## Notes for facilitator Maelezo kwa ajili ya mkufunzi:

**Tunajifunza nini?**

**Hesabati, sayansi na fizikia:** Kujifunza kuhusu ujazo, vipimo, kiwango, na pia kuhusu vimiminika na maada.

**Uchunguzi na majaribio:** Jinsi gani ujazo na kiwango hubadilika kutoka kwenye chombo kimoja hadi chengine.

**Uratibu wa mwili na stadi za misogeo:** jinsi ya kumimina kimiminika kwa umakini kutoka katika chombo kimoja hadi chengine.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

### Tunajifunza nini?

**Kujifunza kupitia michezo:** Watoto hujifunza vitu vingi kupitia michezo, ikiwemo jinsi ya kutatua changamoto na kupitia vitu na watu. Watoto wanapotengeneza vitu kwa kutumia vifaa wanavyoviokota katika mazingira yao, hutumia ubunifu na fikra.  Kitu chochote kwao ni cha kuchezea.

**Kushirikiana na wengine:** Pale watoto wanapocheza na wenzao, hufanya mazoezi ya kuzungumza na kujifunza jinsi ya kushirikiana na kupanga zamu.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

### Tunajifunza nini?

**Kuaminiana na uhusiano chanya:** Watoto wanapopendwa na kujisikia wapo salama, hujifunza kuwaamini watu walio karibu nao na kujenga uhusiano bora kadiri wanavyokua kiumri.

**Kujiamini na kujithamini:** Watoto wananpopendwa na kujihisi wapo salama, hujiamini na kujaribu kubuni vitu vipya, hujieleza na kukuza hisia zao za kujiamini.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

**Tunajifunza nini?**

**Uratibu wa viungo:** kukuza uwezo wa kujizuia na kuratibu mwenendo wa viungo, hukuza ufahamu kwa ujumla, afya na uwezo wa mtoto kujihusisha na michezo.

**Kujifunza kupitia mazingira:** Husaidia watoto kuyapenda mazingira yanayowazunguka jambo ambalo ni muhimu katika wakati huu ambapo mabadiliko ya tabia nchi yanamuarthiri kila mtu.

**Kufurahi tukiwa peke yetu:** Ni muhimu watoto kufurahia wanapocheza peke yao au kwa kujumuika na watu wengine; hii hukuza uwezo wao wa kujitegemea na kutumia vitu vinavyowazunguka.



## Maelezo kwa ajili ya mkufunzi

### Tunajifunza nini?

**Hesabati na kuhesabu:** michezo ya kuhesabu kama vile ya kucheza kwa zamu husaidia kukuza uwezo wa kufanya hesabu za msingi, zikiwemo kujumlisha, kutoa na kuzidisha.

**Ubunifu na uvumbuzi:** Kubuni michezo mipya na kanuni kwa michezo mipya husaidia kukuza uwezo wa kutatua changamoto na kutafakari kwa kujenga hoja, stadi ambazo ni muhimu katika nyanja zote za maisha.

# Kielelezo 3.2a: Mzunguko wa ubaguzi


**Tukiwa watoto**: Tunapokea kilicho mbele yetu na kile tunachoambiwa (kuhusu jinsia, wakimbizi, watu wenye ulemavu, n.k). mf. wanawake hawawezi kufanya kazi za aina fulani, baadhi ya wakimbizi ni 'waporaji wa ardhi', baadhi ya watu wenye ulemavu hawawezi kujifunza.

**Tukiwa vijana:** tunaangalia jamii inayotuzunguka na 'kuthibitisha' kwamba mitazamo yetu ni sahihi, mf. Tunaona kuna wanawake wachache katika sekta fulani kama vile uhandisi, **wakimbizi** wanapewa fursa za bure za kupata ardhi na huduma za umma, watu wenye ulemavu wanatengwa skuli.

**Tukiwa watu wazima:** Hujiaminisha kwa kuegemea mitazamo yetu ya kibaguzi, na kuanza kutenda kwa mujibu wa kile tunachokiamini; tunawalea watoto wa kike kwa kuwaandaa kufanya kazi fulani, tunawaangalia wakimbizi kama **wanufaika wasiostahiki**, tunajitenga na watu wenye ulemavu na familia zao. Tunapotekeleza tunachokiamini, tunaishia **kubagua**.


Matendo ya mtu mmoja mmoja huanzisha na kudumisha **mfumo kandamizi** ambao huunda sera, mazingira na taasisi ambazo huyabagua makundi mbali mbali. Children are born into this and the cycle starts again/ Watoto huzaliwa na kuyakuta haya na kuanzisha (kuendeleza) upya mzunguko wa ubaguzi.

## Kielelezo 3.2b: Mzunguko wa ubaguzi



[**Maelezo ya picha**: Katika ukurasa uliopita tuliona mchoro wenye picha nne na kila picha imeunganishwa na picha nyengine kwa mshale. Maelezo ‘mzunguko wa ubaguzi’ yameandikwa kati kati ya mchoro. Picha iliopo juu ya mchoro inamuonesha mtoto wa kike aliyevaa mtandio mwekundu kichwani akisafisha sakafu ya chumba huku ndoo ikiwa kando yake. Kuna sofa nyuma yake na picha mbili zilizotundikwa ukutani, moja ikiwaonesha watu wanne (watu wazima wawili na watoto wawili) na nyengine ikiwaonesha watoto wawili. Mtoto wa kiume anapita karibu na mtoto wa kike ambae anasafisha sakafu. Amevaa sare za skuli na amebeba mkoba wa skuli mgongoni. Mtoto wa kike anamuangalia. Anaonekana amehuzunika. Picha ya upande wa kulia inawaonesha watoto wanne wakiwa darasani. Watoto wa kike wamevaa mitandio meupe wamekaa pamoja na wanaangalia picha katika kitabu. Picha iliopo katika kitabu inamuonesha mwanamke akiwa anapika na mwanamme aliyefunga tai huku ameshika begi la ofisini. Muonekano wa sura ya mtoto wa kiume na wa kike unaonesha hali ya kuchanganyikiwa au mshangao. Picha iliopo chini ya mchoro inamuonesha mtoto wa kike aliyebeba mtoto mgongoni na amesimama nje ya jengo. Nyuma ya picha kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli wakiwa karibu na jengo. Picha iliopo upande wa kushoto wa mchoro inamuonesha mwanamke akiwa amevaa shungi jekundu kichwani akiwa amekaa juu ya kiti anakata mboga zilizopo kwenye sufuria. Mtoto mdogo wa kike amekaa kwenye kiti kando yake, nae pia anakata mboga. Sura ya mtoto wa kike inaonesha hana furaha. Sura ya mama yake inaonesha kukata tamaa au mwenye hofu. Wamenyamaza. Karibu yao kuna sufuria.]


# Kielelezo 4.1: (a) Vipengele vya mfumo wa elimu




[Picha ya 1: Kioo cha kinakilishi (kompyuta) na baobonye vikiwa kando ya karatasi zenye maandishi.]



[Picha nambari 2: Rundo la vitabu vikubwa vikiwa mbele ya mtu aliyevaa tai aliyechomoza ambae yupo nyuma ya meza.]




[Picha nambari 3: Kikundi cha watoto watano na vijana kikijumuisha mwanamke na wanaume, mtu mmoja akiwa kavaa miwani myeusi huku kashika fimbo na mwengine kashika magongo ya kutembelea, na mwanamke ambae kavaa hijabu.]



[Picha nambari 4: Mtu aliyekaa mezani akiwa kashikilia kalamu iliyowekwa juu ya karatasi akiangalia chini. Kuna saa ukutani.]




[Picha nambari 5:  Mabunda mawili ya noti ambazo zina alama ya dola za kimarekani juu yake.]





[Maelezo ya picha: Upande wa kushoto kuna jengo la ghorofa tatu likiwa na madirisha mengi na alama mbele yake inayoashiria kuwa ni ‘Chuo Kikuu’ na upande wa kulia kuna majengo mawili ya chini yakiwa na mapaa ya bati na milango mitatu iliyofunguliwa katika kila jengo, yakiwa na alama ilioandikwa ‘skuli’]





[Picha nambari 7: Marundo mawili ya karatasi. Moja likiwa na maandishi yanayosomeka ‘SHERIA’ na jengine likiwa na maadishi yanayosomeka ‘SERA’.]



[Picha nambari 8: Picha ya mwanamke akiwa kashika fimbo ndefu iliyoelekezwa kwenye ubao ulio na maandishi.]




[Picha nambari 9: Kikundi cha watu saba akiwemo mwanamke aliyemshika mtoto, mwanamke aliye kwenye kiti mwendo, mwanamme mrefu aliyefunga tai na mwanamme mfupi mkakamavu, mwanamke wa tatu na mzee aliyeshika fimbo ya kutembelea.]



[Picha nambari 10: vitabu vitatu, kimoja kikiwa kikubwa kuliko vyengine na kitabu chengine kilichobanwa kwa spiringi, rula, penseli, kalamu na kifutio (raba).]

[Mchoro unaofuata kwenye ukurasa mwengine unaonesha picha kumi tofauti (Vipengele vya Mfumo wa Elimu) ambavyo vimeelezwa kwa kutumia maneno na picha ambazo zimezunguka maneno ‘Mfumo wa elimu’. Kuanzia upande wa kulia kutokea juu mfano wa kwanza ni picha nambari 1: Kioo cha kinakilishi na baobonye vikiwa kando ya rundo la karatasi zenye maandishi yanayosomeka ‘takwimu za elimu’. Picha zilizosalia zimewekwa katika mpangilio huo huo kama ilivyoelezwa hapo juu. ]

## Kielelezo 4.1: (b) Vipengele vya mfumo wa elimu




## Kielelezo 4.1: (c) Kuunganisha na sekta nyengine





[Maelezo ya picha: Picha inaonesha mchoro wenye maneno ‘Sekta ya elimu’ katika kisanduku kilicho katikati yam choro na mistari inayounganisha kisanduku cha kati na visanduku vyengine vinavyozunguka kisanduku hiki cha kati. Visanduku vinavyoanzia juu kuelekea kulia vinajumuisha mambo yafuatayo; 1. Afya, Marekebisho, 2. Ajira, biashara, maendeleo ya kiuchumi, 3. Ustawi wa jamii, mfumo wa mafao, 4. uhamiaji, wakimbizi, 5. Usafirishaji, 6. Michezo na utamaduni, 7. Idara ya mahakama.]

# Kielelezo 5.2: 'changamoto' za mfumo wa elimu




[Picha nambari 1 Mtoto wa kiume aliyevaa sare za skuli, huku amebeba begi akipanda ngazi. Kwenye ngazi limeandikwa neno 'SEKONDARI'. Watoto watatu wamesimama chini ya ngazi. Akiwemo mtoto mmoja wa kiume ambae anamuangalia mtoto mwengine wa kiume akielekea juu, mtoto mwengine wa kiume akiwa amevaa miwani myeusi, ameshika fimbo akielekea upande mwengine na mtoto wa kike akiwa amebeba mtoto mgongoni huku akiwa na huzuni na akiangalia upande mwengine. Chini ya ngazi limeandikwa neno 'MSINGI'.]





[Picha nambari 2: kuna vyoo viwili, kimoja cha wanawake na chengine cha wanaume.Watoto 10 wa kike na 10 wa kiume akiwepo mmoja anaetumia gongo la kutembelea na mwengine mwenye ulemavu wa ngozi, wakiwa wamesimama kwenye foleni wakisubiri zamu yao kutumia maliwato (choo). vyoo vyenyewe vimechakaa. Upande wa kushoto kuna mtoto akijisaidia haja ndogo kichakani. Jengo la skuli lipo kwa nyuma.]




[Picha nambari 3: Mtoto wa kiume amekaa kwenye kiti mwendo, akiangalia chini. Kuna ngazi ndefu ya kupanda ili kufika darasani. Mwalimu anaonekana akiwa darasani anaendelea kusomesha.]




[Picha nambari 4: Mwanamke amesimama mbele ya wanafunzi ambao wamekaa katika madawati. Anaonesha juu, anazungumza huku akiwa amewaelekezea mgongo wanafunzi. Katika mstari wa mbele darasani kuna mwanafunzi mmoja anaangalia nje kupitia dirishani na mwengine amejiinamia.]




[Picha nambari 5: Rundo la vitabu vitatu, rula/mstari, penseli, peni na kifutio, vyote vikiwa vimezungushiwa duara na mstari uliokatisha kati kati ya duara.]





[Picha nambari 6: mtoto wa kike aliyebeba mtoto mgongoni na amesimama nje ya jengo. Nyuma ya picha kuna watoto wawili wa kike waliovaa sare za skuli wakiwa karibu na jengo. Nyuma kabisa kuna mwalima alivaa shungi jekundu anaonekana akiingia darasani katika jengo lilipo kushoto. Pia kuna mtoto wa kiume alivaa sare za skuli pamoja na mkoba mgongoni anaonekana akielekea katika jengo lilipo upande wa kulia. Kuna mwanamume anaonekana anatembea katika uwanja wa kuchezea.]



[Picha nambari 7: Darasa lililojaa wanafunzi kupita kiasi. Mwalimu anaonekana kwa mbali akiashiria kitu ubaoni. Kuta za darasa na madirisha ni chakavu.]




[Picha nambari 8: Picha mbili zikiwa zimepambanuliwa (kutenganishwa) na mstari. Picha ya kushoto inaonesha jengo lenye maneno yanayosomeka SERA ZA ELIMU. Jengo lipo nyuma ya uzio wa waya. Kupitia dirishani kunaonekana marundo ya karatasi zilizotawanyika. Picha ya upande wa kulia inamuonesha mwanamke na mwanamme wakiwa nje ya nyumba ilioezekwa kwa nyasi Mikono yao ipo hewani ikiashiria kutofahamu jambo fulani. Juu ya mkeka kuna mtoto aliyelala ambae ana mguu mmoja].



[Maelezo ya picha: Mtu mzima mwanamme amekaa mbele ya zunna lililowekwa kwenye meza ndogo. Mtoto wa kiume akiwa amevaa sare za skuli amechukua karatasi mkononi akijaribu kumkabidhi. Mtu aliyekaa anaonekana kuzipuuza na kurusha mikono hewani. Sura yake inaonesha ameghadhibika.]



[Maelezo ya picha: Watoto wanne wamekaa darasani. Watoto wa kike wa kike waliovaa mashungi meupe wamekaa pamoja na wanaangalia picha iliopo kwenye kitabu. Picha ilipo katika kitabu inamuonesha mwanamke akiwa anapika na mwanamme aliyefunga tai huku akiwa amechukua begi la ofisini. Sura ya watoto wa kike zinaonesha kuchanganyikiwa au mshangao.]

# Kielelezo 6.2: Kutumia picha kutafakari elimu mjumuisho

Maelezo yaliopo chini ya picha yanaeleza kile kilichooneshwa kwenye picha, kwa mujibu wa mpiga picha aliyepiga picha hizo.



- Hii ni barabara hatari ambayo wanafunzi wanapaswa kukatisha ili wafike skuli.
- Madereva huendesha kwa kasi sana. Madereva wanapaswa kuelekezwa kupunguza mwendo wanapokaribia eneo la skuli.

[Maelezo ya picha: Watoto watatu wa kike wakiwa wameshikana mikono. Wanakatisha barabara. Gari linakaribia na lipo karibu sana na watoto]



- Maeneo ya skuli kama kilivyo kichochoro/ koridoo hii ni kikwazo kwa ujumuishi, ambapo baadhi ya wanafunzi wanaweza kuwatishia wengine ambao ni wadogo na/au dhaifu.

[Maelezo ya picha: Watoto wawili wa kiume wamesimama kwenye koridoo nyembamba yenye giza.]



- Maji safi, salama na yanayofikiwa yanahitajika. Bila ya maji wanafunzi wanasema hawawezi kumaliza vyema siku, hawawezi kutafakari, hawawezi kunawa mikono baada ya kujisaidia, jambo ambalo hupelekea wapate maradhi, magonjwa, n.k.
- Ardhi inayozunguka mfereji sio tambarare, kwa hivyo maji hayafikiwi na wote, mf. Hayawezi kufikiwa na wanafunzi wasioona na wale wanaotumia viti mwendo.

[Maelezo ya picha: Ndoo mbili za chuma zikiwa zimejazwa maji zipo chini ya mfereji. Ardhi inayozunguka mfereji ni ya udongo ikiwa na mawe makubwa.]



- Wanafunzi wanafanya kazi shirikishi wakijadili sifa zinazoifanya elimu kuwa jumuishi. Ni dhahiri kuwa wanafunzi wa kiume hawashirikishwi katika mjadala na mwalimu wao wa kike, na baadhi yao wanaonekana kuchoshwa.

[Maelezo ya picha: Watoto wa kike na wa kiume wamezunguka meza, huku watoto wengine wakiwa wamesimama nyuma yao. Mwalimu wa kike mwenye tabasamu anazungumza na baadhi ya wanafunzi wa kike ambao wanacheka. Wanafunzi wa kiume wanasikiliza/wanatazama lakini hawacheki.]



- Baadhi ya wanafunzi walipiga picha hii kuonesha ni jinsi gani muda wa kucheza ni muhimu kwao – ni kikwazo katika ujumuishi pale baadhi yao wasipoweza kucheza.
- Ufikiwaji mzuri – ni muhimu kuwa na uwanja tambarare wa kuchezea.

[Maelezo ya picha: Kuna uwanja mkubwa, tambarare uliozungukwa na miti. Wanafunzi wengi wanakimbiakimbia hapo na kucheza.]




- Kuna maliwato mengine kwa ajili ya watoto wa kike ambayo hayaonekani katika picha.
- Wanafunzi waliopiga picha hizi wamefurahi kwa sababu sasa wana choo – kabla ilikua ni ardhi tupu bila mahali pa kujisaidia.

[Maelezo ya picha: Kuna eneo kubwa la wazi lililo tambarare. Ni ardhi tupu isiyo na mimea. Majengo matatu tofauti ya vyoo yamejengwa upande mmoja wa eneo hilo. Kila jengo lina matundu mawili ya kujisaidia.]



- Vitabu visivyofikika: Wanafunzi hawawezi kuvifikia kwa urahisi kwa sababu ya mahali na jinsi vilivyowekwa. Hakuna maandishi ya nukta nundu, ni vitabu vyenye maandishi ya kawaida (vilivyochapwa) pekee.
- Kuwa na vitabu vya kutosha ni jambo zuri kwa sababu wanafunzi hawatohitaji kitabu kimoja kutumiwa na mwanfunzi zaidi ya mmoja.

[Maelezo ya picha: Kuna makabati matatu ya vitabu. Marundo ya vitabu/vijitabu vimekaliana kwenda juu. Makabati yamejaa. Hauonekani mgongo/jina la kitabu.]

# Kitini 7.2: Kushughulikia changamoto za vikwazo katika elimu mjumuisho kupitia igizo-dhima

## Igizo-dhima: Kipindi kinachoruhusu upigaji simu katika redio jamii

### Maelezo

Mama ambae ni kijana akiwa na mtoto mwenye uoni hafifu amekwenda kwenye kituo cha redio jamii akiwa na huzuni. Mama aliwaeleza kwamba alijaribu kwenda kumuandikisha mwanawe katika skuli jirani, lakini mwalimu mkuu ijapokuwa alionesha kumuhurumia, alisikitika kwamba hawezi kumsajili kwa sababu skuli yake haina nyenzo kwa mtoto mwenye tatizo la uoni hafifu. Kituo cha redio kiliwasiliana na jumuiya ya wilaya ya NUDIPU  na kuwaomba iwapo wanaweza kutoa wawakilishi wanne ili washiriki katika kipindi kitachoruhusu simu ili kuhamasisha kuhusu elimu jumuishi katika jamii. Walimuomba mama wa mtoto na mwalimu mkuu kushiriki katika kipindi nao walikubali.

### Waigizaji

- **Watangazaji kutoka katika kituo cha redio jamii (watangazaji 2).** Watangazaji ni vijana wadogo ambao hawana uelewa mkubwa kuhusu elimu jumuishi, lakini wana hamu ya kutengeneza kipindi kizuri, kwa hivyo kazi yao ni kuongoza majadiliano kwa usawa. Wana jukumu la kuongoza kipindi – hii ikimaanisha kutambulisha kipindi, kuwapa nafasi washiriki kuzungumza na kudhibiti maswali ambayo wasikilizaji watauliza.
- **Mama:** Mama wa mtoto alipata ujauzito akiwa bado mdogo na akalazimika kuacha skuli. Ijapokuwa anampenda sana mwanawe, lakini pia anajisikia huzuni kwamba alilazimika kukatisha masomo baada ya kupata ujauzito na ana hamu kubwa ya kuona binti yake akipata elimu bora. Pia ana hamu ya kumuona binti yake akihudhuria skuli na kuwa sehemu ya jamii.
- **Baba:** Baba wa mtoto ni dereva wa boda boda na kipato chake hakitoshelezi kukidhi mahitaji ya familia. Ijapokuwa anampenda sana binti yake, lakini hadhani iwapo binti atamudu kujifunza skuli na anahisi ni vyema wangedunduliza pesa ili wamudu kumsomesha mtoto wao wa kiume ambae hana ulemavu na ambae anatarajia kuanza masomo mwakani.

- **Mwalimu Mkuu:** Amefanya kazi kwenye sekta ya elimu kwa miaka 30 na ana uzoefu wa kutosha**.** Hata hivyo, kwa uzowefu wake anaamini kuwa watoto wenye ulemavu wanapaswa kuandikishwa katika skuli maalumu na kwamba skuli za kawaida hazina nyenzo zinazohitajika ili kukidhi mahitaji ya mtoto  mwenye ulemavu. Anaamini kwamba hili ni jukumu la serikali na sio skuli, na serikali isipoweza kuwapatia fedha za ziada, skuli haiwezi kupokea watoto wenye ulemavu.
- **Jumuiya ya watu wenye ulemavu:** Jumuiya hii imeanzishwa hivi karibuni. Hii ni mara ya kwanza kushiriki katika kipindi kama hiki cha redio na wanataka kukitumia kipindi hiki kama fursa ya kuanza kujenga uelewa kuhusu umuhimu wa elimu jumuishi katika wilaya yao.
- **Wasikilizaji/wanajamii:** Yeyote anaesikiliza anaweza kupiga simu. Kama ilivyo katika jamii yoyote kuna watu wenye mitazamo tofauti, ikiwemo mtazamo tofauti kuhusu elimu mjumuisho. Wasikilizaji watafakari kwa makini na watathmini mitazamo hii kupitia maswali watakayouliza.

## Maswali kwa ajili ya mjadala

- Nini kilikuvutia katika igizo?
- Baada ya kusikiliza maswali yalioulizwa kwa njia ya simu, unadhani kuna kikwazo kipi kikubwa kinachoikabili elimu jumuishi?
- Unadhani ujumbe gani kuhusu elimu mjumuisho zilifanikiwa vyema?
- Kuna yeyote kati ya ‘waigizaji’ ambae alibadili msimamo kuhusu elimu mjumuisho wakati wa igizo? Kama yupo ni yupi? Na jambo gani lilipelekea wabadili msimamo wao?
- Je! Hii inaweza kutokea katika maisha halisi?

**Kielelezo 8.1: Vichwa vya habari vya magazeti**

| |
|---|
| **Mwalimu mkuu amtimua mwanafunzi baada ya kubaini ni mjamzito!** |
| **Wanakijiji wampiga mtoto kwa kuiba!** |
| **Wazazi waandamana baada ya watoto wao wa kike kukatazwa kuvaa mitandio skuli!** |
| **Walimu waandamana kupinga sera ya kukomeshwa kwa adhabu ya bakora – wadai adhabu hiyo ni muhimu kudumisha nidhamu darasani!** |

# Kielelezo 10.2: Fomu ya hatua (Hatua zilizokubaliwa)

| Je, hatua hii itatuwezesha kusikiliza kwa umakini kile watu watakachosema (KUSIKILIZA)? | |
|---|---|
| · Kama ndio itafanyikaje? | |
| · Kama hapana, tubadilishe nini katika hatua hii ambacho kitatusaidia kuwasikiliza watu vyema katika jamii? | |
| **Je, hatua hii itatuwezesha kuwafikia watu mbalimbali katika jamii (WENYE MITAZAMO TOFAUTI NA IMANI)?** | |
| · Kama ndio, itafanyikaje? | |
| · Kama hapana, tubadilishe nini katika hatua hii ambacho kitatusaidia kuwasikiliza watu tofauti katika jamii? | |

| Tunahitaji ujuzi upi ili tuweze kutekeleza hatua hii (UWEZO WETU) | |
|---|---|
| | |
| **Tuna ujuzi huu katika taasisi yetu?** | |
| · Kama ndio, ni jinsi gani tutahakikisha tunatumia ujuzi huu ipasavyo? | |
| · Kama hapana, tunaweza kutafuta njia ya kupata ujuzi huu au tunahitaji kubadilisha mbinu kwa kufanya kile tunachokiweza? | |